# Kutoka Utumwa Hadi Uhuru



**Mapambazuko ya Siku Mpya**

# Kutoka Utumwa Hadi Uhuru

Na F. T. Wright
Kimehaririwa na Andreas Dura

**Mapambazuko ya Siku Mpya**

# From Bondage to Freedom

# In Kiswahili

Mafungu yote ambayo yamewekewa neno (KJV) yametafsiriwa kutoka Biblia toleo la Mfalme James, yaani King James Version.

**Kimechapishwa na:**

Kanisa la Kiadventista la Pumziko la Sabato
(Sabbath Rest Advent Church)
S. L. P. 3699,
Dodoma, Tanzania.

**Simu namba:**
+255-754-275-078 na +255-712-612-613

**Barua pepe:**
srac.tanzania@yahoo.com

Toleo: Marchi, 2011

**Head Quarter:**

Sabbath Rest Advent Church
Waldstraße 37
D-57520 Dickendorf
Germany

E-mail: Sabbath@sabbath-rest-advent.org
Website: www.srac.de

# Dibaji

Chapisho hili ni toleo lililokuzwa la lile ambalo lilinakiliwa kutoka katika tepurekoda ya somo lilitolewa na mwandishi mnamo mwaka 1965 nchini Australia. Wasikilizaji walibarikiwa mno kiasi kwamba waliomba somo hilo litolewe katika mfumo wa maandishi. Mwishowe ilikubaliwa kwamba maandishi ya muda yachapwe moja kwa moja kutoka katika tepurekoda pamoja na marekebisho machache ili kuyaboresha. Hili lilifanywa na kutolewa likiwa na kichwa, *Kutoka Utumwa Hadi Ukombozi*.

Takribani miaka kumi baadaye mwandishi alianza kazi ya kuandika mapitio kamili ya maandishi yale ya awali. Tangu wakati ule kiasi kikubwa cha uzoefu kimepatikana katika ufundishaji wa somo hili, na maisha baada ya maisha yametoa ushuhuda wa uhakika wa upatikanaji wa ushindi kwa wote watakaozitumia kanuni hizi kwa uaminifu. Huenda msomaji anaweza kupata wazo kwamba uzoefu huu wa ukombozi ni kwa ajili ya washiriki hai wa kanisa pekee, lakini kwa kweli unaweza kupatikana kwa watu wote bila kujali wanakotoka. Toleo hili jipya, lililokuzwa lilichapishwa likiwa na kichwa kilichobadilishwa kidogo, *Kutoka Utumwa Hadi Uhuru*.

Kutokana na kumalizika kwa vitabu vilivyochapwa, bila kukidhi mahitaji, imekuwa ni muhimu kuchapa toleo jipya. Toleo hili jipya limebadilishwa kidogo ili kuendana na ufahamu ulioongezeka wa ujumbe huu.

# Yaliyomo

1. Utangulizi……………………………………………………………………………9

2. Sehemu ya 1: Tatizo…………………………………………………………………11

3. Sehemu ya 2: Suluhisho………………………………………………………………25

4. Sehemu ya 3: Baada ya Kuzaliwa Upya……………………………………………39

5. Katika Hitimisho……………………………………………………………………43

# Utangulizi

Kila chapisho hutolewa kwa kusudi fulani. Kusudi la kijitabu hiki ni kuonyesha jinsi ya kupata ushindi dhidi ya matatizo yanayodumu kuchafua uzoefu wa maisha ya watu leo.

Kusudi lake siyo kukuelezea jinsi tabia yako inavyotakiwa kuwa. Kuna hitaji dogo sana kwa hilo. Watu wengi tayari wanajua vile wanavyopaswa kuwa na wanajitahidi kufikia lengo hilo. Kwa wale ambao ni washiriki wa kanisa lililo na maadili na kanuni za hali ya juu, utambuzi wa vile ambavyo tabia zetu zinapaswa kuwa upo wazi zaidi. Si tu kwamba utambuzi huu upo wazi zaidi, vilevile uhitaji wa mtu mwenyewe kufikia ukamilifu huo hushinikiza zaidi.

Tatizo ni hili: Ninawezaje kufikia kiwango ninachojua kuwa ni sahihi? Ninawezaje kupata kile ninachotamani zaidi ya vingine vyote? Hilo ndilo swali ambalo maelfu yasiyohesabika ya watu leo wanauliza kwa dhati.

Iwapo haya ndiyo maswali unayouliza, basi kijitabu hiki ni kwa ajili yako. Hii siyo nadharia ya mtu ambaye alikuwa ameketi tu na kuwazia juu ya njia ya ushindi. Badala yake, ni uwasilisho wa njia ya ukombozi kutoka katika utumwa wa dhambi wa mmoja ambaye, baada ya kutafuta kwa dhati kufikia kiwango cha juu cha maisha ya Ukristo, hatimaye alifanikiwa. Si tu kwamba njia hii imejaribiwa na kuthibitishwa, bali pia ni njia ya Kibiblia. Zaidi ya hayo, imethibitishwa kufanya kazi katika uzoefu wa watu wengine wanaopambana, kama ilivyomfanyia mwandishi.

Ni ombi letu la dhati kwamba itakufanyia kile ambacho imetufanyia sisi.

Wachapishaji

**Sehemu ya 1**

# Tatizo

Leo dunia yote inakabiliwa na matatizo ya kutisha, na watu mahali pote wanatafuta masuluhisho kwa bidii. Lakini chanzo cha matatizo yote, yawe ya kimazingira, uhalifu, ugaidi, uchumi, n.k., hupatikana ndani ya mwanadamu. Na kuna sehemu moja tu ambapo mwanadamu anaweza kupata suluhisho la kuridhisha na la kudumu kwa matatizo haya. Sehemu hiyo ni katika Neno la Mungu aliye hai. Sababu ya ukweli huu, ni kama Petro na Yohana walivyotangaza kumhusu Yesu Kristo: "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." *Matendo* 4:12.

Kwa hiyo, si kwa wanasaikolojia au madaktari, au wanasosiolojia, au wanasayansi, au kwa yeyote kama hao, ambaye tunaweza kwenda kwake kwa ajili ya kupata masuluhisho kwa matatizo haya. Ipo sehemu moja tu ambayo inafunua uweza wa Yesu Kristo unaookoa, nayo ni Neno la Mungu. Ni hapa tu ndipo tunaweza kujifunza jinsi uweza huu unaookoa unavyoweza kuwa wetu binafsi na kupata matokeo yanayotakiwa.

Katika Neno hilo tunao ushuhuda wa kusisimua wa Paulo ambaye kwa maisha yake mwenyewe alijua uweza wake unaookoa, akiwa na maarifa haya alitangaza, "Kwa maana siionei haya Injili." *Warumi* 1:16. Kulikuwa na sababu nzuri sana kwamba ni kwa nini hakuionea haya Injili, sababu ambayo alikuwa na haraka kuitoa: "Kwa sababu ni uweza wa Mungu." *Warumi* 1:16.

Fikiria yote ambayo Paulo angeweza kudai injili hiyo kuwa. Angeweza kuiita nadharia, hoja, habari njema, au mengine kama hayo. Lakini hakutumia hata mojawapo ya fasili hizi. Alitangaza kuwa injili "ni uweza wa Mungu." Kwa Paulo ilikuwa ni uweza, lakini si tu uwezo wowote ule. Ilikuwa ni uweza wa Mungu.

Ni muhimu kwamba mwanzoni kabisa tuelewe injili ni nini hasa. Tutafanya vema kutafakari ukuu na utukufu wa uweza huo. Ilikuwa ni kwa uweza wa Mungu kwamba mbingu na nchi ziliumbwa. Kweli na tarakimu nyingi za kinajimu kuhusu ukubwa wa anga zinatupatia nafasi ndogo ya kuona uweza mwingi wa Mungu.

Uweza ambao Mungu aliutumia katika kuiumba dunia ni uwezo ule ule ambao sasa umetolewa kwa ajili ya wokovu wetu kupitia injili. Kwa sababu, kama Paulo anavyoendelea kusema, "Ni uweza wa Mungu uuletao wokovu." *Warumi* 1:16. Fungu hili halielezi bayana, kwamba injili inatuokoa kutoka katika nini, lakini Maandiko mengine yanaliweka swala hili wazi. Kwa mfano, akiongea kumhusu Mariamu, malaika wa Bwana alitabiri, "Naye atazaa Mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, Yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao." *Mathayo* 1:21 (*KJV*).

Tunapolinganisha maandiko haya tunaona kwamba kusudi la injili ni kutuokoa kutoka katika dhambi. Watu wengi hawajali kuhusu tatizo la dhambi. Wanaishi kufuatana na tamaa zao na Bwana anawapa uhuru kamili kufanya hivyo. Lakini ukweli unabaki pale pale kwamba wao bado ni wenye dhambi.

Kinyume chake, wapo wale wanaojitahidi kubadilika kufuatana na mfano wa uungu. Watakapoushikilia uweza wa injili kwa imani iliyo hai, watabadilishwa kabisa ndani yao kiasi kwamba upendo, uvumilivu, na usafi zitakuwa ni hali zao za kawaida. Watapata uzoefu wa utendaji wa uweza mkuu wa Mungu ndani yao, na watatambua kwamba hakuna uwezo duniani na wala kuzimu ambao unaweza kuwalazimisha kutenda dhambi. Wanajua kwamba hawahitaji kutenda dhambi kabisa. Wanaweza kuishi maisha ya ushindi mkamilifu dhidi ya dhambi zote zinazofahamika kwa kuushikilia uweza unaookoa wa Mwenyezi Mungu.

Ingawa injili ni kwa ajili ya kila mtu, lakini si uwezo wa Mungu kwa kila mtu.

"Kwa maana siionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia." *Warumi* 1:16.

Ni kwa anayeamini tu kwamba injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kutoka katika dhambi. Kwa wengine wote, ni nadharia, hadithi, fundisho, au mengine kama hayo. Kwa anayeamini tu, ni uweza wa Mungu.

Katika fungu linalofuata, Paulo anaendelea kutueleza matokeo ya uweza wa injili, "Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, 'Mwenye haki ataishi kwa imani.'" *Warumi* 1:17.

Ndani ya injili haki ya Mungu mwenyewe inadhihirishwa. Je, neno "inadhihirishwa" lina maana gani katika muktadha huu?

Lina maana kwamba haki ya Mungu inafunuliwa ili ionekane wazi. Lakini injili ya Kristo inadhihirishwa wapi? Inadhihirishwa katika maisha ya wale ambao wamepata uzoefu wa utendaji wake. Na imedhihirishwa pia katika maisha ya Kristo mwenyewe, ambapo ulikuwa ni uweza wa Mungu ambao ulimwokoa Yeye dhidi ya kutenda dhambi kila siku ya maisha yake katika dunia hii. Katika maisha yake, haki ya Mungu imedhihirishwa ili wote wapate kuiona.

"Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake." *1Petro* 2:21. Kama vile haki ya Mungu ilivyodhihirishwa katika maisha ya Kristo kupitia uweza wa injili, vivyo hivyo inatakiwa kudhihirishwa katika maisha ya wafuasi wake leo.

Kadri tunavyoyatazama Maisha hayo na kuona mtiririko usiokoma wa upendo, rehema, neema, uvumilivu, na kila wema mwingine wa Kikristo, kwa asilia tunatamani kuiga kielelezo hicho cha ukamilifu. Lakini maisha ya kushindwa na kupingwa katika siku zilizopita mara nyingi hukatisha tamaa wazo kwamba hilo linawezekana wakati wowote. Hata hivyo, imani yetu inatakiwa kufahamu ukweli mkuu kwamba injili hasa ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kutoka katika dhambi, ili kwamba haki ya Mungu iweze kudhihirishwa katika maisha yetu. Baada ya hapo, ndipo tutakuwa na tumaini lile la ajabu la ushindi dhidi ya kila dhambi kupitia uweza wa Yesu Kristo Mwokozi wetu.

Hii basi, ndiyo injili. Ni uweza ambao Yesu anautumia kuitimiza ahadi yake ya kumtwaa mtu kama alivyo—mpotofu, mchafu, mpungufu; aliyejaa uharibifu, anayedhania wengine uovu, aliye na chuki na matunda yote ya asili ya uovu—, kuiondoa asili ya dhambi; na kisha kuujaza utupu kwa upendo, furaha, amani, upole, unyenyekevu, uvumilivu, na matunda yote ya Roho, ili kwamba haki ya Mungu iweze kudhihirika katika maisha.

"Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama." *Ezekieli* 36:26. Hii ndiyo injili, na hakuna nyingine ila hiyo ambayo inaweza kwa uaminifu kuitwa injili ya Yesu Kristo.

Lakini je, huu ndiyo uzoefu wa Wakristo wengi leo? Je, huu ni uzoefu wako?

Jiulize kwa uaminifu, "Je, ninatenda dhambi kila siku?"

Iwapo jibu lako ni "Ndiyo", basi unafanya nini kuihusu?

Je, unaiungama dhambi hiyo na kumwomba Bwana akusamehe?

Sasa, ni nini kinachotokea baada ya hili? Je, dhambi hiyo inakuwa ni kitu cha kale, au bado ingali pale? Kwa maneno mengine, je, unajikuta ukitenda dhambi ile ile tena na tena?

Unaweza kushangazwa na swali kama hilo, kwani Wakristo wengi wanafikiri kwamba, kwa kuwa sisi ni wanadamu tu, tunapaswa kupambana dhidi ya dhambi zile zile kwa kadri tunavyodumu kuwa hai. Kwa kweli, inakubalika kwa ujumla kwamba tunatenda dhambi zile zile tena na tena, na kwa hiyo tunatakiwa kuziungama tena na tena. Je, uzoefu huu unaweza kuitwa ukombozi kutoka katika dhambi? Jibu liko wazi, Hapana! Huu ni uzoefu wa kutenda dhambi na kuungama, kutenda dhambi na kuungama, kutenda dhambi na kuungama. Lakini siyo ukombozi.

Fikiria nyuma kuhusu uzoefu wako mwenyewe na dhambi kuu inayokusonga katika maisha yako. Fikiria jinsi ambavyo umeitenda, ukaona masikitiko kwa sababu ya hatia, ukamtafuta Bwana kwa ajili ya msamaha, ukaomba kwa dhati msaada wake akuokoe ili usiirudie tena, ukaahidi kwa uaminifu kwamba hautaifanya tena, kisha baadaye ukajikuta unaitenda tena, na tena, na tena, licha ya ahadi zako. Je, si kweli kwako, kama kwa wengine wengi, kwamba dhambi ile ile ambayo ilikuwa ni tatizo lako kuu miaka kumi iliyopita bado ingali nawe?

Iwapo kwa uaminifu wote unaweza kutambua kwamba hivi ndivyo ilivyo, basi umepiga mojawapo ya zile hatua za kwanza kuelekea ukombozi. Si mapenzi ya Bwana kwamba tunaswe katika mzunguko wa kurudia dhambi ile ile tena na tena. Na haitakuwa hivyo katika maisha ya muumini yeyote ambaye amepata uzoefu wa utendaji wa injili kama uweza wa Mungu uuletao wokovu.

Makanisa mbalimbali ya leo yanashikilia mafundisho tofauti tofauti ya imani, na kila moja linadai kwamba mafundisho yake ndiyo sahihi. Lakini haijalishi mafundisho hayo ni sahihi kiasi gani, iwapo hatuelewi na kupata uzoefu wa uweza wa injili unaookoa, basi tumepotea kama vile ambavyo tungekuwa iwapo tusingeamini chochote kabisa. Si nadharia ya dini, kanuni ya imani, mfumo fulani, au kanisa maalumu, ambavyo huleta wokovu, bali ni ukweli unaofanya kazi ndani ya mioyo yetu. Kitu chochote pungufu ya hiki hakitatusaidia. Kwa hiyo, ni lazima tujue kile ambacho injili ya Yesu Kristo inaweza kukifanya katika maisha yetu, na baadaye kuhakikisha kwamba tunaitumia.

Wale tu walio na ushindi binafsi dhidi ya dhambi, wanaojua kwa nafsi zao nini maana ya kuokolewa kutoka katika dhambi zao, na ambao wanaona ukuaji halisi katika maisha yao, hao ndiyo walio na injili ya Kristo. Na ni pale tu tunapopata uzoefu wa utendaji wa injili ndipo tutaweza kuihubiri. Vinginevyo maneno yetu yatakuwa kama shaba iliayo au upatu uvumao. (tazama *1Wakorintho* 13:1)

Jambo muhimu linalotakiwa kueleweka katika hatua hii ni kwamba, kazi ya wokovu inahusisha ushirikiano wetu wa kiakili. Kuna kazi ambayo Mungu pekee anaweza kuifanya, na kuna kazi ambayo lazima tuifanye. Mungu anajua sehemu yake ni ipi, na yupo tayari na radhi kuifanya muda wowote na mahali popote. Lakini hawezi kufanya sehemu yake isipokuwa tumefanya yetu.

Ukweli kwamba tunayo sehemu ya kufanya unathibitishwa na maneno yafuatayo ya Kristo, "Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." *Yohana* 8:32.

Kusudi halisi la kijitabu hiki ni kuweka wazi ukweli ambao tunapaswa kuufahamu, na ambao utatuweka huru. Na tunataka kuonyesha njia hii kutoka utumwa hadi uhuru kwa uwazi na kwa urahisi kadri tunavyoweza.

**Dhambi ni Nini?**

Katika utafutaji wetu wa kuelewa suluhisho la Mungu kwa ajili ya hitaji letu, swali la kwanza ambalo lazima liulizwe ni hili, "Dhambi ni nini?" Swali siyo "Matendo ya dhambi ni nini?" ila "Dhambi ni nini?" Tunajua kwamba matendo ya dhambi yanahusisha uuaji, uongo, wizi n.k, lakini je, tunafahamu dhambi ni nini hasa? Tunahitaji kufahamu jibu kwa hili, kwa sababu ni pale tu tunapolielewa tatizo kwa usahihi ndipo tutakapotafuta suluhisho linalostahili.

Wakristo wengi wanajiamini kwamba wanafahamu jibu la swali hili. Wanapoulizwa, wanajibu kwa haraka, "Dhambi ni uasi." *1Yohana* 3:4.

Jibu hili la Maandiko bila shaka ni sahihi. Lakini tunahitaji kuelewa yote ambayo fungu hili linasema hasa, na si tu ufahamu wetu finyu kulihusu. Neno "uasi" kwa kawaida hubeba wazo la kitendo. Kwa maneno mengine, ufahamu wa kawaida wa fungu hili ni kwamba dhambi ni tendo baya. Yeyote anayefanya tendo baya huchukuliwa kuwa na hatia mbele za Mungu, na kwa hiyo anahitaji tiba ya Mungu, ambayo ni msamaha. Hii inaonyeshwa katika mchoro ufuatao.




Lazima tujue kwamba kitendo ni dhambi kabla hatujahisi hatia. Na ni pale tu tunapotambua hatia yetu ndipo tutatafuta msamaha. Kwa hiyo, ni muhimu sana tufahamu dhambi ni nini, ili tupate tiba ya Mungu kwa ajili yake.

Lakini jibu lililotolewa hadi hapa halina kina cha kutosha kutuhakikishia wokovu kutoka katika dhambi. Ni kweli kwamba dhambi ni kile tunachotenda. Lakini pia ni zaidi ya hicho. Kile tunachotenda ni udhihirisho tu wa tatizo kubwa zaidi. Kile tunachotenda ni tunda la jinsi tulivyo. Ni muhimu kwamba tupate ufahamu huu wa kina kuhusu fasili ya dhambi, kabla hatujaweza kuwekwa huru kutoka katika uwezo wake.


Katika mjadala mmoja na Mafarisayo, Yesu aliweka wazi mbele yao fasili iliyo wazi ya dhambi. Alisema, "Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru." Watu hawa walidhihirisha kutojua kwao kanuni za msingi za tatizo la dhambi kwa kujibu, "Sisi tu uzao wa Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wowote; nawe wasemaje, 'Mtawekwa huru?'" *Yohana* 8:33. Katika jibu lake, Kristo alionyesha kiini cha tatizo, na maneno yake yanatupa ufahamu wa kina kuhusu fasili ya kina kwamba dhambi ni nini: "Amin, amin, nawaambia kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." Tazama *Yohana* 8:32-34.

**Dhambi ni Bwana**

Hapa dhambi inatambulishwa wazi kama kitu kilicho zaidi ya kitendo tu—ni bwana wa mtumwa. Iwapo mweye dhambi ni mtumwa wa dhambi, basi dhambi ni lazima iwe bwana wa mwenye dhambi. Ili kuwa bwana kama huyo, dhambi lazima iwe ni uwezo, kwa kuwa hakuna hata mmoja anayeweza kutawala bila kuwa na uwezo wa kufanya hivyo, hasa wakati watawaliwa wanapokuwa hawako radhi kutoa huduma yao. Dhambi huwalazimisha watumwa wake kuitii, na kwa hiyo tunaweza kuifikiria kama bwana wa mtumwa.

Hivyo fasili yetu ya dhambi lazima sasa ipanuliwe kama ifuatavyo: Dhambi ni bwana anayetutawala kinyume cha nia zetu. Kwa maneno mengine, tupo katika hali ya utumwa. Kwa tatizo hili, radhi, au msamaha, kama ambavyo neno hili linavyoeleweka kwa kawaida, hautoshi. Kile tunachohitaji sasa ni ukombozi, kama mchoro unaofuata unavyoeleza.

Kama ilivyo kwenye msamaha, ndivyo ilivyo kwenye ukombozi—hatuupokei isipokuwa tumeuomba. Lakini, kamwe hatutaomba iwapo hatutambui kwamba hakika tupo katika utumwa. Na wala hatutatambua kwamba tupo katika utumwa iwapo hatutaelewa asili ya dhambi kama bwana wa mtumwa juu yetu. Kwa hiyo, ni wazi kwamba hatua ya kwanza kabisa kuelekea ukombozi kutoka katika dhambi ni kupata picha kamili kwamba dhambi ni nini.




Cha kusikitisha ni kwamba, ufahamu wa watu wengi unaishia kwenye hatua ya: Kitendo—Hatia—Msamaha. Hii, ina maana kwamba, kamwe shoka haliwekwi kwenye shina la mti. (Tazama *Mathayo* 3:10.) Bwana wa mtumwa haondolewi na kule kukiri dini—kupatana kwa nje na matakwa ya dini—hukubalika kuwa kitu halisi.

Bwana wa mtumwa amepewa majina kadhaa katika Biblia. Katika *Warumi* 8:7 huitwa "nia ya mwili"; katika *Warumi* 6:6 huitwa "utu wetu wa kale"; katika *Ezekieli* 11:19 huitwa "moyo wa kijiwe". Pia hufananishwa na ukoma.

**Sheria Inaingia**

Lakini hakuna mahali pengine ambapo utendaji wa bwana-dhambi unaelezewa vizuri zaidi ya *Warumi* 7. Tutaanza katika fungu la 9, ambapo tunasoma, "Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria; ila ilipokuja ile amri, dhambi ilihuika, nami nikafa." Hapa Paulo anarejea katika wakati fulani ambapo sheria iliingia katika maisha yake. Akizungumza juu ya muda kabla hajaelewa kwamba amri zinafika mpaka kwenye mawazo na makusudi ya moyo alisema, "Nami nalikuwa hai hapo kwanza bila sheria." Kwa maneno mengine, alikuwa ni mwenye dhambi wa hiari. Hii ndiyo hali yetu kabla hatujaijua sheria ya Mungu. Tuko radhi na wenye furaha kabisa kuwa wenye dhambi, hata kama huenda hatujifikirii kuwa hivyo. Hali yetu haitutii wasiwasi.

Lakini wakati huja ambapo sheria huingia katika uzoefu wetu. Nayo huleta maarifa ya madai ya haki ya Mungu kwa maisha na tabia zetu, na ni uzoefu huu ndiyo hufanya hatua ya kwanza kabisa kuelekea kwa Kristo. Sheria inaweza kutujia kupitia usomaji wa Neno, kupitia kwa mhubiri, au njia nyingine, lakini ni lazima itufikie iwapo tutampata Kristo kama Mwokozi kutoka katika dhambi.

Maarifa ya sheria ya Mungu hutuongoza zaidi—kwenye maarifa ya vile tulivyo mbele za Mungu. Huu ni uhakikisho wa dhambi. Ni hatua ya pili muhimu kuelekea kwa Kristo.

Uhakikisho, baadaye, huongoza kwenye toba, alimradi hatuuzimishi kwa kuipinga kazi ya Roho Mtakatifu katika mioyo yetu. Hili linaweza kutokea, kwa kuwa siyo uzoefu wa kupendeza kujiona wenyewe kama Mungu anavyotuona. Mwelekeo wa asili wa ubinadamu wetu ni kukataa ufunuo huo kama kitu kisichotakiwa. Mfano kuhusu mwelekeo huu unapatikana katika kisa cha Feliki na Drusila kama kilivyoandikwa katika *Matendo* 24:24–27. "Na Paulo alipokuwa akitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja, Feliki akafanya hofu akajibu, 'Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita.'" Fungu la 25.

Ukweli kwamba Feliki alipata hofu, ni ushahidi wa wazi kwamba alipata uhakikisho wa kina. Hili lingemwongoza kwenye toba iwapo asingeupuuza ufunuo usiopendeza wa nafsi yake. Lakini alimwondoa mtume Paulo katika muda halisi ambao alihitaji zaidi huduma yake kumwongoza, hatua kwa hatua, kuelekea kwa Bwana. Hivyo sisi pia tunahitaji kuwa makini sana ili tusije tukaikataa picha ya kweli ya jinsi tulivyo wakati Bwana anapoionyesha kwetu kupitia chombo chochote anachokichagua. Iwapo tutaipokea, atatupatia roho ya toba wakati tunapoiomba.

### Toba

Toba ni nini? Toba ina maana zaidi kuliko watu wengi wanavyoielewa. Toba si tu kuhuzunika kwa sababu ya dhambi, bali pia kugeuka na kuiacha moyoni. Haitoshi tu kuhuzunikia mateso ambayo dhambi inaleta—yaani matokeo ya dhambi yetu. Yuda na Balaam walifanya hivyo tu, na walishindwa kupata uzoefu wa toba ya kweli. Tunahitaji kwenda zaidi ya hapo. Lazima tuone jinsi ambavyo dhambi inatutenga na Mungu na ina maana gani kusimama mbele zake katika hali hiyo. Kama vile tunavyochukia uchafu kwa sababu ni uchafu, vivyo hivyo tunatakiwa kujifunza kuichukia dhambi kwa sababu ni dhambi. Kufanya hivi itamaanisha pia kwamba tutaipenda haki kwa sababu ni haki.

Kwa namna yoyote, siyo hali ya asili kwetu kuichukia dhambi na kupenda haki, wala hatuwezi kuizalisha sisi wenyewe. Kwa hiyo Mungu, kupitia wema wake, anatupatia toba kama kipawa. Maandiko yanautangaza ukweli huu katika maneno yafuatayo: "Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi." *Matendo* 5:31. Tazama pia *Warumi* 2:4.

Mara tu baada ya toba kupokewa kama kipawa kutoka kwa Mungu, kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu kupitia Neno lake, hufuatiwa na ungamo la dhambi.

Hizi, basi, ndizo hatua nne za kwanza kuelekea kwa Kristo: maarifa, uhakikisho, toba, na ungamo. Tunaweza kufikiri kwamba tumepata uzoefu wa hatua hizi na kudhani kuwa tuko katika uhusiano mwema na Mungu. Lakini je, tumewekwa huru mbali na tatizo la dhambi? Iwapo bado linadumu kuwepo, ni kwa sababu kipo chanzo cha msingi ambacho bado hakijashughulikiwa. Uzoefu wa pekee wa kweli katika hatua hizi nne za kwanza utaambatana na ukombozi kutoka katika dhambi.

### Maarifa ya Ile Kweli

Hebu tuchunguze uzoefu wetu tulipokuja kwenye maarifa ya kweli ya Mungu kwa mara ya kwanza. Pasipo shaka ukweli huo ulionekana kuwa wa kupendeza na unaopatana, lakini pia ulipaswa kuleta uhakikisho. Katika nuru ya wema wa Mungu, maisha yetu yaliyopita yanaonekana kujazwa na ubinafsi na dhambi. Uhakikisho huu unakusudiwa kufanya toba ya kina ndani yetu ili kwamba tusitamani kitu kingine zaidi ya kuondolewa dhambi yetu. Kama Waisraeli wa zamani walivyosema, "Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii." *Kutoka* 24:7, vivyo hivyo tunadhamiria kugeuka na kuacha dhambi na kutii amri za Mungu.

Baadaye kunakuwepo kipindi cha mafanikio, kama tabia ya nje inavyohusika. Ushindi mkuu unaweza pia kupatikana dhidi ya ile mivuto ya dunia ambayo hapo awali ilitushinda. Lakini kwa namna fulani, matatizo ya ndani kama vile kukosa uvumilivu, hasira, n.k. huendelea kuwepo. Haya huinuka juu na kutuangusha. Kisha tunapiga magoti chini ya uhakikisho wa kina wa dhambi inayoendelea kutusonga. Tunaziungama dhambi na kudhamiria kwamba kuanzia hapo na kuendelea itakuwa tofauti—lakini haiwi hivyo. Shida zile zile zinajitokeza tena na tena. Uzoefu wetu unakuwa ni ule wa kujaribu na kushindwa, kuungama na kujaribu na kushindwa tena.

**Uzoefu wa Paulo**

Hii ndiyo picha halisi ambayo mtume Paulo anaishuhudia katika *Warumi* 7:15–24. "Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri ile sheria ya kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, lipo lililo baya. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani. Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili yangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, masikini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?"

Katika maneno haya, Paulo anatupatia maelezo ya kufaa sana ya uzoefu wa wengi wa wanaokiri kuwa watoto wa Mungu. Na mtu kama huyo anaweza kusikika akisema, "Hiyo ni picha halisi ya uzoefu wangu, Paulo alikuwa anaandika kunihusu mimi wakati alipoandika maneno hayo."

Tunapochunguza maandiko haya, tunaweza kuona kwamba Paulo alipata uzoefu wa hatua zote hizo nne. Anakiri mara kwa mara, kwamba amepungua kwa matakwa ya sheria, kitu kinachoonesha kwamba aliijua sheria na hali yake mwenyewe kuhusiana nayo. Mwanzoni katika sura hii aliishuhudia moja kwa moja katika maneno yafuatayo, "Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema." *Warumi* 7:12.

Tena anasema, "Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni." Fungu la 14. Tumekwisha kuona kwamba ujuzi wa sheria huongoza kwenye ujuzi wa nafsi zetu wenyewe. Hivyo mara tu baada ya kusema, "Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni," Paulo anakiri kwamba, "bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi." Bila shaka, Paulo alipokea pia kipawa cha toba katika hatua hii kwani aliichukia dhambi, kama anavyosema mwenyewe, "Bali lile nilichukialo, ndilo ninalolitenda." *Warumi* 7:15, 19. Zaidi ya hayo, toba yake inaambatana na ungamo la dhambi. Kwa kweli mafungu haya yote ni ungamo.

Hivyo tunaweza kuona kwamba, katika hatua hii ya utafutaji wa wokovu Paulo kwa hakika amepitia uzoefu wa hatua hizi nne za kwanza kuelekea kwa Kristo: maarifa, uhakikisho, toba, na ungamo. Lakini wakati huo huo, ni wazi kwamba hana ukombozi kutoka katika dhambi.

Ni muhimu tuweze kuuona ukweli huu. Kwani iwapo tunafikiria kuwa tumepitia katika hatua hizi na hivyo tuko salama, basi tupo katika hatari kubwa ya kutopata ukombozi kutoka katika dhambi. Lakini uzoefu wa Paulo, kama unavyoelezwa katika *Warumi* saba, unatuonyesha wazi kwamba inawezekana kupitia hatua hizi, angalau kwa kiwango fulani, na bado tuwe ni watumwa wa dhambi—yaani tuwe bado katika uhitaji wa ukombozi kutoka katika uwezo wa bwana-dhambi ambaye anatutawala kinyume cha nia zetu. Ni utumwa huu ambao unatuweka katika hali ya kutenda dhambi na kutubu, kutenda dhambi na kutubu dhambi zile zile zinazotusumbua siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka. Ni maisha ya utumwa wa dhambi, hata kama tunaweza kujua vizuri na kutamani kutenda mema kwa moyo wetu wote.

Tunapofikia maarifa ya kweli ya Mungu kwa mara ya kwanza, na kupata uhakikisho wa dhambi, na kisha kuitubu, na kuiungama, tunao mwelekeo wa kuamini kwamba tumepokea wokovu. Ushuhuda wa Paulo katika *Warumi* saba huonekana kwetu kama uthibitisho kwamba hivi ndivyo ilivyo. Na hata hivyo, bado tunaweza kuwa katika utumwa wa utu wetu wa kale wa dhambi.

Kwa kawaida, kutokana na ushuhuda wa Paulo wa uzoefu wake katika *Warumi* saba, tunaweza kuhitimisha kwamba amekwisha kuupata wokovu. Tunaweza kutoa sababu kama ifuatavyo: Paulo alikuwa mtu mkuu wa Mungu. Aliielewa injili na mpango wa wokovu. Atakuwepo katika Ufalme, japokuwa bado anashuhudia kwamba alikuwa mtu wa mwilini, ameuzwa chini ya dhambi na mtumwa wa dhambi. Hakuweza kutenda lile alilojua kwamba ni jema, lakini alijikuta mwenyewe akifanya lile ambalo alijua kwamba ni ovu. Iwapo huu ulikuwa ni uzoefu Paulo, basi lazima tutarajie kwamba uzoefu wetu wa Ukristo utakuwa sawa

kama alivyoeleza katika *Warumi* saba. Kwa maneno mengine, uzoefu wa mtu wa *Warumi* saba ni uzoefu wa mtoto wa Mungu aliyezaliwa upya.

Lakini swali la msingi ambalo tunatakiwa kujiuliza ni hili: Je, Paulo alikuwa anaelezea uzoefu wake kama ulivyokuwa baada ya kuwa Mkristo, au alikuwa anaelezea kile alichokipitia kabla hajawa Mkristo mshindi?

**Mtu wa Warumi Saba**

Ili kutoa kielezo kwa suala hili, nitasimulia uzoefu niliowahi kuupata wakati fulani. Nilikuwa nimekaribishwa kuzungumza kuhusu njia ya ukombozi kwa mtu ambaye alishikilia nafasi ya juu katika ofisi ya kanisa. Alikuwa ni meneja wa taasisi ya kidini, aliyejifunza vizuri mafundisho ya kanisa hilo, bila shaka aliishika sheria kama matakwa ya nje yalivyohusika. Kwa miaka alikuwa akisimama mimbarani kuwahubiria watu. Lakini bado nilipomsomea maneno ya Paulo katika *Warumi* saba aliniambia, "Hiyo ndiyo picha halisi ya uzoefu wangu tangu nilipojitoa kwa Bwana. Nilizaliwa nikiwa na laana ya hasira na bado ninalo tatizo hilo. Mimi hukasirika. Kisha ninajisikia uhakikisho wa dhambi hiyo. Ninaiungama na kuazimia kwamba haitatendeka tena. Lakini jaribu linapokuja ninaingiwa na hasira tena na tena na tena. Kwa hakika ninaweza kuhisi hali ya Paulo katika sura hii."

Mtu huyu alisema kweli na kuwa wazi kama Paulo katika *Warumi*. Bila kumhukumu, ni muhimu kuuliza, je amepata uzoefu wa ukombozi kutoka katika dhambi, kama unavyoahidiwa katika neno la Mungu?

Kabla ya kujaribu kulijibu swali hili, tunapaswa kuwa na uhakika kwamba tunaelewa kwa uhalisi kwamba uzoefu wa mtu huyu ni nini: Anaijua sheria ya Mungu na anaishika kwa kadri anavyoweza. Ni mwaminifu katika kuhudhuria kanisani kila wiki na anashikilia ofisi ya juu katika kanisa. Anatoa sadaka kila siku. Anashiriki katika utendaji wa mipango ya kimisionari ya kanisa lake na anaheshimiwa sana na jamii. Lakini anashuhudia kwamba bado ni mtumwa wa asili yake ya ndani na hawezi kufanya mambo yale ambayo anajua katika moyo wake kwamba anapaswa kuyafanya na anajitahidi kwa bidii kuyafanya.

Huyu ndiye mtu halisi wa *Warumi* saba. Yeye siyo mwenye dhambi wa hiari duniani anayejali kidogo sana mambo ya Mungu na ya umilele. Tunajua kwamba mtu wa dunia, iwapo atadumu kuwa hivyo, hawezi kuokolewa. Lakini vipi kuhusu mtu wa *Warumi* saba? Hili ndilo swali, na ni muhimu kwa mafanikio yetu ya umilele kwamba tulifahamu jibu lake sahihi.

Hata hivyo zipo, sababu nyingine mbili ambazo zinaweza kutushawishi kwa nguvu, kusema kwamba huu ni uzoefu wa mtoto halisi wa Mungu. Kwanza, kuna ushuhuda wa maisha yetu wenyewe, ambayo yanafanana na maelezo ya *Warumi* saba. Tunapotafakari juu ya kujinyima kwetu kote ambako tumefanya kwa ajili ya ukweli tunaweza kusita kukubali kwamba yote hayo ni bure.

Kisha tena tunawafikiria wale wapendwa waliokufa na ambao tunajua kwamba walikuwa katika uzoefu wa *Warumi* saba. Tunahifadhi kwa upendo mkubwa matumaini kwamba tutawaona tena mbinguni. Lakini iwapo mtu wa *Warumi* saba si mtoto wa Mungu, basi tunahofu kwamba hatutawaona tena.


Tukiwa na vishawishi hivi binafsi vikifanya kazi katika akili zetu, lazima tuelewe kwamba si matumaini yetu wala hofu zetu ambazo zitabadilisha ukweli wa suala hili hata kidogo.

Hivyo swali linabaki mbele yetu katika umuhimu wake wote: Je, uzoefu ulioandikwa katika *Warumi* saba unaelezea uzoefu wa mtoto wa kweli wa Mungu au la?

Kuna uwezekano wa majibu matatu kwa swali hili. Kuna wale wanaosema kwa upesi kwamba ameokolewa. Kisha wapo wale ambao hawana uhakika. Na mwisho, wapo wengine wanaosema kwamba mtu huyu kwa hakika hajaokolewa.

Kwa hiyo ni wazi kwamba yapo maoni tofauti iwapo mtu wa *Warumi* saba anawakilisha uzoefu wa wale wanaookolewa au wale wanaopotea. Lakini ni dhahiri pia kwamba lazima tuujue ukweli juu ya suala hili. Iwapo tunaamini kwamba mtu wa *Warumi* saba anafurahia uzoefu wa Ukristo, kwa hakika hatutatafuta kitu kingine zaidi. Lakini iwapo, kwa upande mwingine, sivyo, basi ni lazima tutafute suluhisho la Mungu kwa tatizo hili. Suala hili ni la muhimu mno kwetu kubaki bila kuwa na uhakika, kwani hatutaki kupita katika maisha haya tukijitegemeza katika tumaini la uongo na kudhani kuwa tupo kwenye njia sahihi wakati kwa kweli sivyo ilivyo.

Tunahitaji kujihadhari na tafsiri na mawazo ya kibinadamu katika kujibu swali hili. Mamlaka pekee katika suala hili ni Neno la Mungu. Tutakapopata jibu pale tunapaswa kuliamini kwa sababu ni Neno la Mungu tulilopewa kwa ajili ya wokovu wetu.




**Mashahidi Watatu**

Tunaposoma maneno ya Paulo, tunaweza kuona kuwa mtu wa *Warumi* saba yupo katika utumwa. Anajua kile anachopaswa kutenda, lakini anakuta kwamba haiwezekani kufanya hivyo. Ni wazi yeye si mwenye dhambi wa hiari, lakini bado ni mwenye dhambi. Anautumikia uwezo wa dhambi, na kwa hiyo, yupo katika utumishi wa Shetani.

Iwapo anamtumikia Shetani, basi hawezi kuwa anamtumikia Mungu, kwani, "Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali." *Mathayo* 6:24.

Iwapo mtu wa *Warumi* saba hamtumikii Mungu, atawezaje kuwa mtoto wa Mungu? Haiwezekani kabisa. Na iwapo yeye siyo mtoto wa Mungu, basi anawezaje kuwa na wokovu? Tena jibu ni kwamba hawezi. Kwa hiyo, kwa msingi wa ushahidi huu, ni wazi kwamba mtu wa *Warumi* saba hana wokovu.

Huu ni ushahidi mmoja kwamba mtu wa *Warumi* saba hana wokovu. Uko wazi na unasadikisha, lakini hautoshi, kwani ni kanuni ya Maandiko kuwa "kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike." *Mathayo* 18:16**.** Kwa hiyo tutaendelea kutafuta ushahidi zaidi wa Biblia.

Katika mafungu ya mwisho ya *Warumi* saba, Paulo anafikia mwisho wa maelezo yake ya kuwa katika utumwa wa uweza wa dhambi. Katika hali ya kukata tamaa isiyo na matumaini alilia, "Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" Fungu la 24.

Ni vizuri katika hatua hii, kuuliza swali lililoelezewa na pia kujibiwa vizuri na Dk. E. J. Waggoner katika kitabu chake, *Christ and His Righteousness*, uk. 86, 87. "Je, Mkristo halisi hupitia uzoefu wa kutisha wa mwili wa mauti kiasi kwamba nafsi hulazimika kulia kwa ajili ya kukombolewa?—Kwa kweli hapana "... Je, Kristo hukomboa kutoka katika uzoefu halisi wa Ukristo?—La hasha. Basi utumwa wa dhambi, ambao kwao mtume analalamika katika *Warumi* saba, si uzoefu wa mtoto wa Mungu, bali wa mtumwa wa dhambi. Ni kwa ajili ya kuwakomboa wanadamu kutoka katika utumwa huu, kwamba Kristo alikuja; si kutuokoa, katika maisha haya, kutoka katika vita na mapambano, bali kutoka katika kushindwa; kutuwezesha tuwe thabiti katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake, ili kwamba tuweze kutoa shukrani kwa Baba ambaye 'alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake,' ambaye kwa damu yake tunao ukombozi."

Suala ambalo E. J. Waggoner analiweka wazi sana hapa ni kwamba Kristo kamwe hawezi kutukomboa kutoka katika uzoefu halisi wa Ukristo. Na hapa yupo Paulo, akiomba kukombolewa kutoka katika uzoefu wa *Warumi* saba. Huu ni ushuhuda wa pili kwamba *Warumi* saba siyo uzoefu wa mtoto wa kweli wa Mungu.

Lakini kilio cha Paulo kwa ajili ya ukombozi kinafanywa kwa imani. Anafahamu kwamba kuna wokovu kwa Mungu pekee, na kwamba injili ni uweza wa Mungu kuokoa kutoka katika dhambi. Kwa hiyo, katika kujibu swali lake, "Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?" anaweza kusema, "Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu!" *Warumi* 7:25. Kisha anapumzika kwa muda wa kutosha ili kutoa jumla ya uzoefu wa *Warumi* saba kwa kuongeza maneno, "Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi." Fungu la 25. Anajua nini kilicho chema, na katika akili yake ameamua kumtumikia Mungu. Anauamini ukweli wa Mungu. Anatamani kuwa mwaminifu kwa Bwana, lakini tabia halisi ya maisha yake imetolewa wakfu kwa utumishi wa dhambi.

Kisha Paulo anaendelea kuelezea hali iliyobadilika baada ya ombi lake kutoka katika moyo uliopondeka kwa ajili ya ukombozi na shukrani kwa kuupokea. "Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti." *Warumi* 8:1, 2.

Kisha, katika sehemu yote iliyobaki ya *Warumi* nane, Paulo anazungumza juu ya uhuru, juu ya ushindi, juu ya kuwa mwana wa Mungu, na hatimaye anamalizia kwa ushuhuda wa ushindi, "Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu." *Warumi* 8:37-39.

### Uzoefu wa Aina Mbili Tofauti

*Warumi* saba ikilinganishwa kwa makini na *Warumi* nane, itaonekana kwamba ni aina mbili tofauti kabisa za uzoefu. *Warumi* saba ni uzoefu wa mtumwa ambaye analazimishwa kuzitenda kazi za dhambi kinyume cha mapenzi yake, wakati ambapo *Warumi* nane ni habari ya mtu ambaye amewekwa huru kutoka uwezo wa dhambi na sasa anaweza kutenda kile ambacho anajua kwamba ni chema na ambacho anatamani kukitenda. Sura hizi zote haziwezi kuwa maelezo ya kweli ya Mkristo aliyezaliwa upya. Wakati ambapo tunaweza kupata ugumu kuona kwamba mtu wa *Warumi* saba siyo mtoto wa Mungu, hatupaswi kupata ugumu kutambua kwamba mtu wa *Warumi* nane ni Mkristo.

Mafungu yafuatayo katika *Warumi* nane yanatuonesha kwamba mtu huyu kwa hakika anafurahia uzoefu wa Ukristo: sasa basi "hakuna hukumu ya adhabu" (fungu la 1); Yuko "huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti" (fungu la 2); haki ya sheria inatimizwa ndani yake, na haenendi "kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho" (fungu la 4); ni mwana wa Mungu na hivyo ni mtoto wa Mungu (fungu la 14-16); kwa hiyo, ni mrithi, na, "kwa hakika", mrithi pamoja na Kristo, (fungu la 17); na ni zaidi ya mshindi kwa Yeye aliyetupenda, (fungu la 37).

Yote haya yanaelekeza kwenye uzoefu halisi wa Mkristo aliyezaliwa upya. Lakini sura hii ya nane ni tofauti kiasi gani na uzoefu ulioelezwa katika sura iliyotangulia. Kwa hiyo, *Warumi* saba lazima iwe ni maelezo ya kitu kingine. Haiwezi kuwa ni maelezo ya uzoefu wa Mkristo. Huu ni ushuhuda wa tatu kwamba mtu wa *Warumi* saba hana wokovu.

Lakini huu siyo ushuhuda wote. Mwishoni mwa *Warumi* saba, Paulo analia ili akombolewe na, hivyo badiliko kuu linapofanyika, anamshukuru Bwana kwalo. Kisha ushuhuda wake ni huu, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." *Warumi* 8:1.

Paulo amekwishaelezea mapito ya uzoefu wa kuogofya wa kuwa katika utumwa kwa nguvu ya dhambi, kulia kwake kwa ajili ya ukombozi, na upokeaji wake. Kisha anatoa hitimisho la mambo yote na kusema kwamba hayuko tena chini ya hukumu adhabu. Kuhakikisha kwamba kila mtu anaelewa ni kwa nini sasa hakuna hukumu ya adhabu, anaendelea kusema, "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti." *Warumi* 8:2.

Awali katika *Warumi* saba, ushuhuda wa Paulo ulikuwa tofauti kabisa. Pale, kwa kweli hakuwa huru mbali na sheria ya dhambi na mauti. Lakini katika *Warumi* nane yuko huru, na kwa sababu yuko huru, hakuna hukumu ya adhabu. Kwa maneno mengine, wakati alipokuwa hayuko huru mbali na sheria ya dhambi na mauti, alikuwa chini ya hukumu ya adhabu.

Kwa namna yeyote ile, hatujamaliza shuhuda zote ambazo zinaelekeza kuwa mtu wa *Warumi* saba hana wokovu, lakini shuhuda hizi zinatosha kabisa kueleza jambo hili.

**Hii Inamaanisha Nini Kwangu?**

Iwapo ukiutazama uzoefu wako kwa uwazi sana, utaweza kuona iwapo unafanana na maelezo yaliyotolewa katika *Warumi* saba au na yale ya *Warumi* nane. Iwapo mtu wa *Warumi* saba ni picha ya hali yako ya kiroho, basi unapaswa kutambua kwamba bado haujapata wokovu kutoka katika dhambi.

Unaweza kuwa mshiriki mwaminifu wa kanisa, unajishughulisha na kazi zake, unaunga mkono kanuni za imani yake, na kwa ukarimu unasaidia mipango yake, na wakati huo kuwa na sifa nzuri kwa watu wanaokuzunguka. Iwapo ni hivyo, ufunuo huu ya kuwa bado upo katika uzoefu ulioelezwa katika *Warumi* saba utakujia kama mshtuko mkali. Lakini ni muhimu sana kwamba uje, kwa sababu tunahitaji kuelewa hali yetu halisi kabla hatujaweza kushikilia kile ambacho Bwana anasubiri kutupatia.

Kuna uwezekano wa aina mbili za mwitikio kwa utambuzi huu. Asili ya kibinadamu huelekea kukataa chochote ambacho kinavuruga mtindo wa maisha ulioimarishwa. Baada ya kuridhika kwa muda mrefu katika faraja ya kufikirika tu kuhusu wokovu, huwa hatuko tayari kuukabili ukweli kuhusu hali yetu halisi. Kwa hiyo, ipo hatari halisi kwamba tutaukataa na kupokea kitu kingine ambacho kinakubalika zaidi na kinachotupendeza.

Iwapo jaribu hili litakushinda, basi hoja kadhaa zitaibuka mara moja katika mawazo kupingana na ushahidi wa Neno la Mungu. Katika hofu yako unaweza kusema, "Kwa nini, mbona mimi ni Mkristo! Tazama yale ambayo nimeacha ili kumfuata Kristo! Tazama ufahamu wangu mpana wa Maandiko, muda ninaotumia kusoma na kuomba, madaraka yangu ya juu kanisani, na ... na ... na ...." Hakuna kosa baya zaidi linaloweza kufanywa kuliko hili. Watu wengi sana wamepoteza uzima wao wa milele kwa sababu hawakuwa na ujasiri na unyofu kukabiliana na ukweli kuhusu nafsi zao wakati ulipowajia. Matokeo yakawa kwamba, Roho wa Mungu hakuweza kufanya zaidi kwa ajili yao, na mvuto huo ukatoweka kabisa.

Mwitikio mwingine ambao unaweza kuupata ni ule wa kukata tamaa kabisa. Iwapo uko mwaminifu vya kutosha kutambua ukweli wa Neno la Mungu wakati unapofunua kwa wazi kwamba hauna wokovu, ni kawaida kabisa kujisikia hali ya kuzidiwa na hisia kuwa umepotea na kuhukumiwa. Unaweza kujiona kana kwamba umetengwa milele na Mungu.

Iwapo hivyo ndivyo unavyojiona, basi kwa hakika hakuna chochote bora zaidi kwako. Ni kupitia tu kwa utendaji kazi wa Roho Mtakatifu, kwamba tunaweza kufikia utambuzi huu. Ni muhimu kwamba tuone hali yetu halisi na kwamba pumbazo la usalama wa uongo livunjwe, kabla Roho wa Mungu kutufanyia kazi inayofuata. Watu wengi mno wanaishi katika hali ya ulaodikia, bila kujua kwamba wao ni wanyonge, wenye mashaka, maskini, vipofu, na uchi. Tazama *Ufunuo* 3:14-22. Kwa hiyo, unaweza kuwa na shukrani kwamba umefika mahali ambapo unajiona mwenyewe kama aliyepotea kabisa.

Unaweza kufurahi pia, kwa sababu Mungu ameandaa njia ya ukombozi kutoka katika uwezo wa dhambi. Hauhitaji kubakia katika uzoefu wa *Warumi* saba; ukiwa umeshindwa na kukatishwa tamaa katika shauku yako ya kweli na ya dhati ya kumtumikia Mungu aliye hai. Njia ya ukombozi siyo siri, na kusudi la kijitabu hiki si tu kufunua tatizo, lakini pia ni kuonyesha njia ya wokovu. Kwa hiyo, vumilia mpaka imani yako itakapoushikilia uweza wa Mungu, na utaokolewa kutoka katika mzunguko wa unyonge wa kuungama na kutenda dhambi tena, na kuponywa.

Tumethibitisha kuwa uzoefu unaoelezwa katika *Warumi* saba kwa hakika, siyo ule wa Mkristo. Sasa tunahitaji kuelewa ni kwa nini mtu kama huyu hawezi kuishika sheria, ingawa anatamani kufanya hivyo. Ufahamu huu ni sehemu ya muhimu ya suluhisho la tatizo.

**Asili ya Mwanadamu**

Ili kuelewa ni kwa nini uzoefu wa *Warumi* saba siyo ule wa Mkristo, tunatakiwa kuelewa asili ya mwanadamu. Ni kweli kwamba sisi ni viumbe wenye sehemu nyingi, kukiwa na

uhusiano wa karibu kati ya viungo vyetu vyote. Hata hivyo licha ya uhusiano huu, tofauti lazima iwekwe kati ya sehemu muhimu, ili kwamba kazi zinazofanywa na kila sehemu zitambuliwe.

Kuwa wazi zaidi, kila mmoja wetu ana akili yenye hekima na inayofikiria, ambayo kwayo tunapokea taarifa kupitia milango mbalimbali ya fahamu: kuona, kusikia, kugusa, kuonja, na kunusa. Ni kupitia fahamu hizi kwamba Mungu huwasiliana nasi ili kutufunulia hali yetu binafsi, hitaji letu, na kile ambacho atatufanyia.

Akili haipokei kila kinachotolewa. Kwa sababu fulani fulani, vitu vingine hukataliwa. Inaweza hata kuukataa ukweli halisi ambao tunauhitaji sana iwapo imefundishwa kuuamini uongo, au iwapo upokeaji wa ukweli huo hauleti raha, utaleta usumbufu, au utatugharimu.

Ili kupokea au kukataa ukweli, akili lazima ifikiri na kufikia mahitimisho. Mahitimisho hayo yanahitaji kufanyiwa maamuzi, ambayo baadaye hudai matendo yanayopatana nayo kwa upande wa mtu binafsi. Huku ndiko kuweka nia.

Wakati kazi hii inapokuwa imekamilishwa katika akili, mwili huamrishwa kutii na kutimiza maamuzi yaliyofanywa. Kwa kweli, mwili umekusudiwa kutimiza makusudi ya akili. Hata hivyo, tunapokuja kujifunza kazi ya matengenezo, ambayo inafuata baada ya uzoefu wa kuzaliwa upya, tutaona kwamba mwili unaweza pia kuishinikiza akili ili kutimiza matakwa yake kwa kujifurahisha au kujilinda nafsi.

Ukweli kwamba mwili ni chombo unawekwa wazi katika maneno haya, "Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki." *Warumi* 6:13.

Kielezo rahisi kitaonyesha kuwa mwili unatakiwa kuwa mtumishi wa akili. Hebu tufikirie kwamba unataka kusafiri kutoka sehemu ulipo kwenda sehemu nyingine. Taarifa zilizohifadhiwa katika akili yako zinakuambia kwamba lazima kwanza utembee kutoka sehemu ulipo sasa mpaka kwenye stesheni ya treni. Akili yako haiwezi kwenda pale peke yake, lakini inaweza kuviamrisha viungo vya mwili, yaani nyayo na miguu, kukuchukua mpaka pale. Kuna matukio mengine mengi ya namna hii katika maisha yetu ya kila siku.

Katika suala la mtu wa *Warumi* saba, mwili haufanyi mara zote kile ambacho akili inataka ukifanye. Hebu tusome tena tamko hili lililo wazi katika fungu la 15: "Maana sijui nifanyalo; kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda."

Chochote ambacho tunakitenda, kinatendwa kupitia viungo vya mwili. Lakini katika suala hili, mwili hautendi kile ambacho akili ya Paulo inatamani ukitende. Badala yake, unatenda kitu kile kile ambacho anakichukia kukitenda. Bila shaka, ni katika akili yake inayofikiri ambapo chuki yake dhidi ya kitu hiki ipo. Ni katika akili yake ambapo anaamua kutokukitenda. Hivyo tunayo hali ambapo akili inajua kile kinachopaswa kutendwa, inatamani kukitenda, na inapeleka maagizo kwa viungo vya mwili kukitekeleza, lakini kwa mfadhaiko mkuu anagundua kwamba mwili unafanya kitu kingine.

Kila mmoja amepitia uzoefu huu wakati mmoja au mwingine. Kwa kweli, iwapo unaweza kushuhudia kwamba bado upo katika uzoefu wa *Warumi* saba, basi unafahamu kikamilifu jinsi hali hii ilivyo. Kwa mfano, unaweza ukawa umedhamiria kutoongea tena kwa haraka au maneno machafu kwa wengine. Uko mwaminifu kabisa katika maazimio yako. Nia imeelekezwa kufanya hili, na kwa muda mambo yote yanaweza kwenda vizuri. Lakini siku inafika ambapo kiungo kile kikaidi, ulimi, hutoa maneno ya kuropoka tena na maneno machungu ya kushtaki. Na baadaye unajisikia majuto na masikitiko kiasi gani.

Bila swali, mtu wa *Warumi* saba anajua kipi kilicho chema. Anaifahamu sheria ya Mungu na anafurahi katika kweli kuu za Neno la Mungu. "Kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati." Fungu la 18.

Swali sasa linaibuka: kwa nini mwili hautii maagizo ya akili? Iwapo tutaweza kugundua sababu ya kutotii huku, tutakuwa karibu zaidi na suluhisho la tatizo.

Hali inayoelezewa katika *Warumi* saba si ya kupendeza wala si nzuri. Mungu hakuiumba miili yetu ili iasi dhidi ya akili zetu. Hapana! Mungu alitupa mwili utimize matakwa ya akili na kuitii nia. Hii sio picha ambayo tunapewa katika *Warumi* saba, lakini katika *Warumi* nane tunamwona Paulo ghafla akiwa anaweza kutenda kile ambacho anajua ni chema.

Katika hatua hii watu wengi wanaweza kudhani kuwa tatizo halisi ni kwamba nia ni dhaifu mno kuutiisha mwili. Wanadai kuwa maazimio na uwezo zaidi unahitajika ili kuuleta mwili

katika utii kwa akili. Iwapo utajaribu suluhisho hili, utagundua kwamba, haijalishi maazimio na nguvu ya nia kiasi gani unajitahidi kuweka, hali haitakuwa bora. Hilo siyo suluhisho la tatizo. Jibu linapatikana katika ufahamu juu ya uwepo wa kipengele cha tatu cha asili ya mwanadamu.

**Sheria ya Dhambi**

Kila mmoja wetu ana akili na mwili, lakini pia tuna kipengele cha tatu kinachofanya kazi ya muhimu katika uzoefu wetu wa maisha. Kipengele hiki cha tatu hakionekani mara moja, na wapo wengi ambao wanakana uwepo wake kama kitu ambacho ni tofauti. Wanafikiri kuwa ni kitu kimoja na kile kile, kama asili ya mwili wa kibinadamu. Hili ni kosa la kutisha kwa sababu, tofauti na asili yetu ya kibinadamu, kitu hiki cha tatu ni adui yetu. Zaidi ya hayo, kukana uwepo wake kama kitu tofauti kutatuzuia kupata ukombozi kutoka kwake.

Utambuzi wa kipengele hiki cha tatu cha uhai wetu ni muhimu kwa kufaulu kwetu katika utafutaji wa ushindi dhidi ya dhambi. Kwa hiyo, sasa tutaangalia uwepo wake, na jinsi kinavyotofautiana na asili ya mwili wetu wa kibinadamu.

Paulo anavitaja vipengele vyote vitatu katika *Warumi* 7:22, 23. "Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani. Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu."

Tunapoangalia fungu hili kwa makini, tunaona kuwa Paulo anaifuraia sheria ya Mungu kwa utu wake wa ndani. Furaha hii inaweza tu kuwa kwenye akili, inayofikiri, kama inavyothibitishwa na fungu lifuatalo: "Lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu ..." Hivyo, wakati katika akili yake, Paulo anaifurahia sheria ya Mungu, katika viungo vyake ipo sheria nyingine inayopiga vita na ile sheria ya akili hiyo. Matokeo yamekuwa ni kwamba amekuwa mateka au mtumwa wa hii sheria ya dhambi.

Tunahitaji kutofautisha kati ya sheria ya dhambi na mwili wenyewe—hivi siyo kitu kimoja. Ingawa sheria ya dhambi siyo mwili, yenyewe inaishi ndani ya huo mwili. Mwanzoni katika sura hii Paulo alisema kwamba, "Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu." Fungu la 17. Maneno yake, "ikaayo ndani yangu," hueleza wazo hili la "kuishi ndani."

Kwa hiyo, hii "sheria ya dhambi" katika viungo vya mwili siyo asili ya mwili wa kibinadamu wa damu na nyama. Ni kitu kingine ambacho kinakaa katika huo mwili na kuutawala, kinyume cha nia ya akili inayofikiri na iliyoelimika. Maandiko mengine pia yanathibitisha ukweli huu. Kwa mfano, "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama." *Ezekieli* 36:26.

Kitu ambacho Paulo anakiita "sheria ya dhambi" katika kitabu cha *Warumi*, kinatajwa kama "moyo wa jiwe" katika *Ezekieli*. Katika *Warumi* saba kitu hiki kinaoneshwa kuwa kinakaa ndani ya mwili, wakati hapa katika *Ezekieli* ahadi ni kwamba kitaondolewa kutoka katika mwili. Kitatolewa nje, na mbali kutoka kwa wale ambao kwao Bwana analeta wokovu. Wakati moyo wa jiwe unaondolewa kutoka ndani yetu, mwili unabaki pale, kwani mwili wenyewe hauondolewi kutoka ndani yetu. Badala yake, ni kitu fulani kinaondolewa kutoka katika mwili. Maneno haya yanaweka wazi kwamba kuna vitu vitatu tofauti: akili, mwili, na sheria ya dhambi, au moyo wa jiwe, ambao unakaa katika huo mwili na kuutawala kulingana na mapenzi yake, kinyume na matakwa ya akili.

Katika *Warumi* 8:7, kitu hiki hiki cha tatu kinatajwa tena kwa jina lingine: nia ya mwili. "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii."

Andiko hili linaongezea ushahidi zaidi, wenye nguvu juu ya uwepo wa kitu hiki cha tatu ndani ya mtu. Iwapo tutaangalia kwa makini kile kinachosemwa katika fungu hili, tunaweza kuona kwamba haliwezi kuhusika na asili ya mwili wa nyama au ya kibinadamu. Kwani, wakati inawezekana kwa mwili wa nyama wa dhambi, ulioanguka kuwa chombo cha haki, kwa kuitii sheria ya Mungu, lakini haiwezekani kwa nia ya mwili kufanya hivyo.

Nia ya mwili si tu kwamba ipo katika uadui na Mungu, yenyewe ni uadui. Umbile lake lenyewe, asili yake, kiini chake, na vyote ambavyo kwavyo imefanyika, kwa yenyewe ni uadui juu ya Mungu. Iwapo ingekuwa tu katika uadui na Mungu, basi ingewezekana

kupatanishwa na Mungu. Lakini wakati ambapo nia ya mwili yenyewe ni uadui, basi haiwezi kupatanishwa na Mungu; haiwezi kamwe kuitii sheria ya Mungu. Hilo haliwezekani.

Ingawa nia ya mwili haiwezi kupatanishwa na Mungu, mwili unaweza. Kwa kweli, katika *Warumi* 6:13, Paulo anamwita mtu aliyeongoka kuvitoa "viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki."

Hivyo, tuna asili moja au nguvu ndani yetu ambayo ni uadui juu ya Mungu na haiwezi kumtumikia, na tuna nguvu nyingine, inaitwa mwili, ambayo inaweza na inapaswa kumtumikia. Nguvu hizi mbili haziwezi kuwa moja au kitu kile kile. Lazima ziwe vitu viwili tofauti, kwani moja haiwezi kutolewa kama silaha kwa utumishi wa sheria iwapo haiwezekani kwake kuitii sheria.

Nia ya mwili ni sheria ya dhambi; ni moyo wa jiwe na nguvu ya dhambi ambayo inatawala katika maisha ya mtu kinyume cha matakwa ya akili. Tatizo si kwamba mwili unaitawala akili, bali ni kwamba huo mwili uko chini ya nguvu nyingine ambayo kwayo unalazimishwa kuitii.

Paulo anatoa muhtasari wa tatizo lote vizuri sana katika fungu la mwisho la *Warumi* saba anaposema, "Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi." *Warumi* 7:25.

Wapo mabwana wawili watendao kazi katika maisha ya mtu wa *Warumi* saba. Mmoja ni Bwana Mkuu wa kweli yote, ambaye kwake akili imejitoa kwa utumishi; mwingine ni sheria ya dhambi, ambaye mwili ni mtumwa wake. Akili na mwili vinatumikia aina mbili tofauti za nguvu, na ni kwa sababu hii kwamba mwili hautendi kile ambacho akili inaueleekeza kufanya. Mwili uko chini ya bwana mwingine, ambaye ni dikteta na adui wa kufisha wa sheria ya Mungu.

Sasa tumefika kwenye kiini cha tatizo: kile ambacho tunatenda ni matunda ya jinsi tulivyo. Kama Yesu anavyosema: "Kwa maana hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya, wala mti mbaya uzaao matunda mazuri; kwa kuwa kila mti hutambulikana kwa matunda yake; maana, katika miiba hawachumi tini, wala katika michongoma hawachumi zabibu. Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake hunena yale yaujazayo moyo wake." *Luka* 6:43-45.

Hapa Kristo anazungumza juu ya kanuni ya maumbile ambayo haijawahi kuvunjika, na ambayo hata mtoto anaielewa. Ni kanuni ya kutegemewa kabisa: Iwapo unataka kupata matunda mazuri, kwanza kabla ya yote lazima uwe na miti mizuri—yaani, aina sahihi ya miti. Baada ya kuzielekeza akili zetu kwenye kanuni hii inayofahamika, baadaye Mwokozi anasema kwamba, kama ilivyo katika maumbile ndivyo ilivyo katika ulimwengu wa kiroho. Kwa maneno mengine, kanuni ile ile inahusika pale. Kwa hiyo, iwapo tunataka kuwa na maisha yaliyojazwa na matendo mema, basi kabla ya yote lazima tuwe watu wema.





**"Je! watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya."** ***Mathayo*** **7:16, 17.**

Lakini hatuwezi kuwa watu wema wakati nia ya mwili, au moyo wa jiwe bado unakaa ndani yetu. Kuwa na asili na uwezo mwovu ndani yetu ni kuwa mtenda dhambi wa asili, na hivyo kwa kawaida kuzaa matunda maovu na siyo mema.

Hili, basi, ndilo tatizo: moyo wa jiwe. Kwa mtu aliye katika *Warumi* saba tatizo siyo akili, kwani imekwisha kuongolewa kwa utumishi wa Mungu, na kwa kweli za Neno la Mungu. Wala tatizo si asili ya mwili wa kibinadamu, kwani wenyewe upo tu katika utumwa kwa nguvu nyingine. Tatizo ni moyo wa jiwe, au sheria ya dhambi—yaani nguvu ambayo inakaa katika viungo na kuvitawala kinyume cha nia.

Hii siyo kusema kwamba akili na mwili haviwezi kuwa tatizo. Vinaweza kuwa, lakini vyenyewe siyo tatizo kuu katika uzoefu wa *Warumi* saba. Tunafikia uzoefu huu kwa sababu tumeona uzuri wa ukweli na kuongolewa nao. Lakini hadi pale mwili wetu utakapokombolewa kutoka kwa uwezo ukaao ndani, hauwezi kamwe kuepuka utawala wa dhambi na kufanya yale ambayo akili inauelekeza kufanya.

Sheria ya dhambi katika viungo ndiyo tatizo kuu. Huo ndiyo mzizi, sababu ya msingi, chanzo halisi cha taabu yote. Kwa sababu hili ndilo tatizo, basi ni wazi kwamba hapa ndipo ambapo suluhisho lazima lifanye kazi. Kwa hiyo, tutaendelea kutafuta na kuelewa ni jinsi gani suluhisho hilo linaweza kutumiwa.

Sehemu ya 2

# Suluhisho

Sasa kwa kuwa tatizo halisi limeshaeleweka, swali ni hili: Tunawezaje kulishughulikia?

Mwanzoni kabisa, hebu tufahamu kwamba jaribio lolote linalofanywa kuilazimisha nia ya mwili kuitumikia sheria ya Mungu ni kujaribu kitu kisichowezekana. Tunapaswa tu kukumbuka mfano wa Yesu wa mti wa miiba katika *Luka* 6:44 ili kutambua kwamba hakuna kiasi chochote cha kulazimisha ambacho kitasababisha matunda mema kuzaliwa kutoka katika moyo ulio mwovu.

Hebu tuutazame mti wa mwiba. Ni kwa asili yake kabisa kwamba upo katika uadui dhidi ya sheria ya uzaaji wa tufaha. Iwapo tunakuta mti wa miiba katika bustani yetu, tunajua kwamba hakuna kiasi chochote cha upaliliaji, umwagiliaji maji, utiliaji mbolea, upogoleaji au uangalizi ambao utazalisha hata tufaha moja kutoka katika mti huo. Tunafahamu bila shaka kwamba hili haliwezi kutendeka.

Tunapotafuta ushindi dhidi ya dhambi, hebu tushawishike vile vile kwamba hakuna kiasi chochote cha juhudi, usomaji wa Neno la Mungu kwa bidii, mahudhurio kanisani, utendaji kazi katika safu za kimisionari, maombi ya dhati, au ukarimu katika matoleo, havitaweza wakati wowote kusababisha nia ya mwili kuzaa matunda ya Roho. Hii siyo njia, kwani "nia ya mwili . . . haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." *Warumi* 8:7. Huu ni ukweli halisi wa maisha kama ilivyo kweli kwa mti wa miiba ambavyo hauitii sheria ya uzaaji wa tufaha, wala kwa hakika hauwezi kuitii.

Kwa hiyo, yeyote aliye na nia ya mwili anayejaribu kuishika sheria ya Mungu, ili kuzaa matunda hai ya Roho, anajaribu kitu kisichowezekana kabisa. Hadi pale hiyo nia ya mwili inaposhughulikiwa, ndipo mtu anaweza kuanza kuishika sheria ya Mungu. Shoka lazima liwekwe katika shina la mti. Hakuna njia nyingine. "Na shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti. Basi mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni." *Mathayo* 3:10.

### Sheria ya Mungu

Katika ulimwengu wa kidini leo, wapo ambao wanafikiri kwamba suluhisho la tatizo hili ni kuitupilia mbali sheria ya Mungu. Lakini hii inawezekana? Iwapo tunajaribu kutatua tatizo la siku yenye joto lisilovumilika kwa kukivunja kipimajoto, je, hili litabadilisha joto au kulipunguza tatizo? Kwa kweli hapana! Tatizo litabaki vile vile, na joto halitabadilika. Kile ambacho tutakuwa tumepoteza ni njia mahsusi inayotuwezesha kujua kiasi halisi cha joto.

Vivyo hivyo, iwapo sheria itaondolewa mbali, haitaleta tofauti yoyote kwa dhambi. Bado itaendelea kuwepo pale pale. Yote yanayotokea ni kwamba tutapoteza kile kinachoonyesha kwa usahihi kwamba dhambi ni nini.

Katika mafungu ya kwanza ya *Warumi* saba, ukweli huu umeelezwa vyema kwa njia ya mfano wa ndoa. Hapa Paulo anaonyesha kwamba hakuna haja ya kuibadili sheria. Yenyewe tayari ni kamilifu na haihitaji kubadilishwa. Anayehitaji kubadilishwa ni mtu, kwani hapo ndipo tatizo lilipo.

"Ndugu zangu, hamjui, (maana nasema na hao waijuayo sheria,) ya kuwa torati [au sheria] humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai? Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa na sheria ya mume. Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine." *Warumi* 7:1-3.

Kila mmoja anafahamu hali hii inayohusu sheria ya ndoa. Wakati mwanamke ameolewa kwa mumewe kwa mujibu wa sheria, sheria itahukumu jaribio lolote la kuolewa na mume

mwingine kama uzinzi. Lakini iwapo mumewe akifa, basi sheria ile ile ambayo hapo awali iliihukumu ndoa yake kwa mume mwingine, sasa itaikubali. Badiliko limetokea, lakini siyo katika sheria. Limetokea kwa mwanamke. Amebadilika kutoka kuwa mwanamke aliyeolewa na kuwa mwanamke ambaye hajaolewa.

Hii pia ni kweli katika ulimwengu wa kiroho. Kwa kweli, Paulo hatoi maelezo marefu juu ya suala la ndoa, lakini anaitumia kama kielelezo cha ndoa ya kiroho pamoja na Kristo.

"Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia sheria, kwa njia ya mwili wa Kristo, ili mpate kuolewa na mwingine, Yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda." *Warumi* 7:4

Hakuna kidokezo chochote katika fungu hili juu ya badiliko lolote linalofanywa katika sheria, lakini kuna badiliko kwa mtu. Hii ina maana kwamba lazima tufe kabla hatujaolewa na mwingine, yaani Kristo, kwani Yeye ndiye aliyefufuka katika wafu.

Kama ambavyo tumekwisha kuona, kusudi ambalo kwalo Yesu Kristo alikuja katika dunia hii ni kutuokoa kutoka katika dhambi: "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, Yeye ndiye atakayewaokoa watu wake *kutoka katika* dhambi zao." *Mathayo* 1:21 (*KJV*).

Kuokolewa kutoka katika dhambi ni kuokolewa kutoka katika uasi wa sheria, kwani dhambi ni uasi wa sheria, kama ilivyoandikwa, "Dhambi ni uasi." *1Yohana* 3:4 . Kuasi sheria ni kutotii. Kwa hiyo, kuokolewa kutoka katika uasi wa sheria maana yake ni kukombolewa ili tutii. Kwa hali yoyote, juhudi ya dhati ya nia, wala kuitangua sheria haviwezi kutuokoa kutoka katika tatizo hili.

**Kung'oa Kabisa**

Kwa kuwa sasa tunafahamu namna ambayo kwayo tatizo haliwezi kutatuliwa, tunageukia suluhisho la kweli—ung'oaji kabisa wa asili ya kale na kuijaza nafasi yake kwa asili mpya. Hili linafundishwa wazi katika Maandiko, kama maneno yafuatayo yanavyoonesha:

"Nami nitawapa moyo mmoja, nami nitatia roho mpya ndani yao; nami nitauondoa moyo wa kijiwe katika miili yao, nami nitawapa moyo wa nyama; ili waende katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyatenda; nao watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao." *Ezekieli* 11:19, 20.

Hapa Bwana anasema wazi kwamba atauondoa ule moyo wa kale, wa dhambi, wa jiwe nje ya mwili wetu na kutupa moyo mpya badala yake. Hasemi kwamba atatupa moyo mpya pamoja na ule wa kale. Hilo halitatenda kazi, wala sivyo fungu linavyosema. Ahadi ni kwamba Mungu atauondoa moyo wa kale kutoka katika miili yetu na kuweka roho mpya na moyo mpya mahali pake.

Kazi ya kung'oa kabisa na kuweka kitu kingine mahali pake ina kusudi maalumu, na imekusudiwa kuleta matokeo fulani. Inafanywa ili "waende katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyatenda; nao watakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wao."

Tumekwisha kuona kwamba sababu iliyomfanya Paulo kushindwa kutenda kile alichotaka ilikuwa ni kwamba alikuwa na nia ya mwili ya kale ikimtawala. Hili pia ndilo tatizo letu wakati tunapokuwa katika uzoefu wa *Warumi* saba. Sasa tunahitaji kuona kwamba Bwana anajua kabisa pale tatizo lilipo, na kwamba yuko tayari kutoa suluhisho kwalo—kuiondoa nia ya mwili na kuweka moyo mpya kabisa badala yake.

Katika mfano wa Kristo wa mti wa miiba, tunapata suluhisho lilo hilo. Mti wa miiba unasimama ukiwa wa kijani na kustawi katika bustani, lakini hauwezi kuzaa tunda lolote. Huziba njia, hutumia udongo mzuri na ukichana nguo za wale wanaopita pembeni yake. Hili ndilo tatizo la mtunza bustani. Anataka bustani yake izae matunda mazuri kama vile tufaha na machungwa, lakini alio nao ni huu mti wa miiba tu. Suluhisho bila shaka ni kuung'oa mti huu wa miiba na mahali pake kupanda mti mzuri. Wakati mtunza bustani anapofanya hili, anajua kwamba kwa wakati ufaao atapata matunda mazuri, kwa sababu rahisi tu kwamba sasa anao mti mzuri.

Vivyo hivyo, mtu wa *Warumi* saba anatamani kuzaa matendo mema ya sheria—matunda ya Roho kama vile upendo, furaha, amani, utu wema n.k. Hata hivyo, yeye ana asili ovu ndani yake ambayo haiwezi kuzaa utii wa upendo, bali chuki, kiburi, wivu, na mengine kama hayo. Yuko katika mashaka yale yale ya mtunza bustani aliyekuwa na mti wa miiba, na suluhisho la tatizo lake pia ni lile lile. Asili ovu lazima ing'olewe kabisa kutoka katika mwili wa kibinadamu na badala yake kuweka asili iliyozaliwa kutoka juu. Na ni kwa kuomba tu

kwamba hili lifanyike ndipo mtu wa *Warumi* saba anaweza kuwa mtoto wa Mungu na baadaye kuzaa matunda mema ya Roho.

Ukweli huu umeelezwa tena na tena katika Maandiko ili kwamba ushahidi uliorudiwa usiache mashaka kuhusu njia ya ukombozi kutoka katika nguvu ya kutisha ya dhambi. "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." *Warumi* 8:2-4.



**Haitoshi tu kuukata mti mwovu. Shoka lazima liwekwe katika shina halisi la mti, vinginevyo utachipua tena.**

Mungu alimtuma Mwana wake duniani ili kuihukumu dhambi katika mwili. Ipo tofauti ya muhimu ambayo inapaswa kuthibitishwa hapa. Ingawa matendo ya dhambi yanaweza kutajwa kama "dhambi za mwili," ni uwezo wa moyo wa jiwe, au nia ya mwili, unaokaa ndani ya mwili, kwa kweli ndiyo "dhambi katika mwili." Yesu hakuja ili kufanya kazi ya juu juu ya kuhukumu tu dhambi za mwili. Alikuja kuihukumu dhambi katika mwili, ambayo ndiyo chanzo halisi cha tatizo. Hiki ndicho chanzo halisi cha uzoefu wa kushindwa tena na tena kwa wale wote ambao bado wana moyo wa jiwe ndani yao.

Ni nini matokeo ya kuihukumu dhambi katika mwili? "Ili maagizo ya haki ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." *Warumi* 8:4. Nia ya mwili imehukumiwa, imeng'olewa kabisa, na kuondolewa kwa kusudi fulani—kutupatia haki ya Mungu kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

### Kifo cha Utu wa Kale

Nini matokeo ya huku kuihukumu dhambi katika mwili? Je, Kristo aliihukumu ili kuitiisha na kuidhibiti? Je, aliihukumu hadi uhamishoni? Je, aliihukumu kwa tamko tu la kutoikubali? Hapana, si hata moja kati ya haya. Yesu aliihukumu dhambi mpaka kifo, kifo ambacho kilifanyika kama matokeo ya kifo chake na kufufuka kwake mwenyewe. Ukweli huu umeelezwa wazi katika *Warumi* 6:1–6.

"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."

Fungu la sita ndiyo kilele cha hoja iliyo katika mafungu haya. Mafungu matano ya kwanza yanawahusu watoto wa kweli wa Mungu walio ndani ya Kristo Yesu, na kwa hiyo wamehesabiwa haki na pia wana haki ya kumiliki ufalme huko juu. Imeelezwa wazi kwamba wamekufa na kufufuka, vile vile kama Yeye alivyokufa na kufufuka. Lakini ni katika fungu la mwisho ndipo tunaambiwa wazi kile ambacho kimekufa.

Kabla hatujaangalia kile ambacho lazima kife kabla hatujawekwa huru kutoka katika dhambi, hebu kwanza tutazame uzito wa ujumbe wa mafungu matano ya kwanza.

Tunaambiwa kwamba ni wale tu ambao wamekufa ndiyo wanaweza kuishi. Ni namna nyingine ya kusema kwamba cha kale lazima kiondoke kabla kipya hakijaja. Kile cha kale huondolewa kwa kifo na kile kipya huletwa kwa ufufuo. Ukweli huu unaelezwa kwa uzito zaidi katika fungu la 5: "Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake."

Sehemu ya kwanza ya fungu hili ni sentensi yenye sharti: "Kwa maana kama tulivyounganika katika mfano wa mauti yake ..." Hii inaeleza ukweli kwamba wakati sharti hilo linapokuwa limetimizwa, mengine yatafuata. Lakini ni wale tu ambao wamekufa pamoja na Kristo ndio wanaoweza kuishi pamoja naye. Hivyo ni kusema, kipya kinakuja tu iwapo kile cha kale kimeondolewa mbali. Mti wa miiba lazima uondolewe mbali kabla mti wa tufaha haujachukua nafasi yake. Haiwezi kukua mahali pamoja.

Ni nini ambacho Paulo anakisema hasa katika mafungu haya? Je, anasema tu maneno yanayovutia na yasiyo na maana, au haya ni maelezo ya uzoefu halisi? Wakati anaposema kuwa tunapaswa kufa pamoja na Kristo, anamaanisha nini? Je, tunatakiwa kufa kweli, au anazungumza tu kuhusu badiliko katika mtazamo wa kiakili?

Kwa watu wengi sana inaonekana kuwa vigumu kuamini kwamba Paulo anazungumza kuhusu kifo halisi. Sababu ya hili inatokana na kushindwa kutofautisha kati ya mwili wa kibinadamu ulio wa dhambi na nia ya mwili (pia inaitwa moyo wa jiwe, mume wa kale, na bwana-dhambi). Tunaelekea kufikiri kuwa asili ya dhambi ni mwili wa kibinadamu, na kwa kuwa tunajua kwamba mtu haukatishi uhai wake katika dunia hii ili kuzaliwa upya, hivyo inadhaniwa kuwa kinachozungumzwa hapa ni kifo cha kufikirika. Kifo hiki mara zote hufikiriwa kuwa ni tukio halisi katika maisha ya Kristo, lakini ni cha mfano tu inapokuja kwa mtu aliyezaliwa mara ya pili.

Ni kweli kwamba hatufi kimwili, wakati tunapoachana na uzoefu wa *Warumi* saba, na kuwa mtoto wa kweli wa Mungu aliyefufuka. Tunakuwa na mwili ule ule wa damu na nyama baada ya kuongoka kama tuliokuwa nao hapo kabla. Hapajakuwepo na kifo au badiliko katika mwili wetu unaoonekana. Mwili wa kibinadamu wa dhambi ni mwili wa kufa. Hakuna ambaye atakombolewa kutoka kwake mpaka asubuhi ile kuu ya ufufuo wakati Kristo atakaposhuka na kuwaita watu wake ili awapeleke katika makazi yao ya mbinguni. (Tazama *1Wakorintho* 15:50–54; *1Wathesalonike* 4:13–17; na *Mathayo* 24:30, 31.)

Bado hata hivyo, lazima tufe ili tuweze kuzaliwa upya, kwani iwapo hatutakufa hatuwezi kuwa ndani ya Kristo. Basi ni sehemu gani ndani yetu inayokufa? Jibu linapatikana katika *Warumi* 6:6. "Tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye..." Hapa kuna jina jipya: "utu wetu wa kale." Je, maneno haya yana maana gani? Ni nani au nini ni utu wa kale? Sehemu ya pili ya fungu inatuambia kwamba utu wa kale ulisulibishwa, "ili mwili wa dhambi ubatilike..." Paulo angeweza kuandika: "Tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili kwamba utu wa kale ubatilike...", lakini badala ya kurudia maneno "utu wa kale" kwa mara ya pili, anatumia jina jingine, "mwili wa dhambi." Hii inatuambia kwamba "utu wa kale" na "mwili wa dhambi" ni kitu kile kile kimoja.

Katika *Warumi* 7:24, tunakutana bado na jina jingine, "mwili huu wa mauti." Hii tu ni njia nyingine ya kuelezea kile ambacho mwanzoni Paulo alikiita "sheria ya dhambi" katika sura hiyo. Kwa hiyo, kutokana na kujifunza kwetu mpaka hapa, tunajua kwamba, "utu wa kale," "mwili wa dhambi," "mwili huu wa mauti," na "sheria ya dhambi," yote haya yanataja kitu kile cha tatu, "nia ya mwili" ambayo "haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." *Warumi* 8:7.

Ni ile "nia ya mwili" ndiyo ambayo husulubishwa katika maisha ya wale wanaoongoka. Ule "utu wa kale" lazima uangamizwe, kwa kifo, kabla uhai mpya haujafufuliwa badala yake.

Hebu tufahamu wazi kabisa kuhusu ukweli kwamba lazima kuwepo na kifo halisi. Kusulubishwa siyo uhamishoni. Na kifo hakimaanishi kuwekwa katika kifungo cha maisha gerezani. Si kufungwa kwa minyororo wala kuwekwa chini ya udhibiti wa mwingine. Kusulubishwa ni aina ya kifo. Kusudi lake ni kuua; na wale wanaosulubisha hawaridhiki mpaka matokeo haya yanapofikiwa.

Kwa hiyo, Paulo anaposema kwamba utu wa kale unasulubishwa, ana maana kwamba unauawa. Kuhakikisha kwamba tunazingatia maana yake, anasema kuwa tunasulubiwa ili mwili wa dhambi uweze kubatilika. Kitu fulani kinapobatilika, kinaangamizwa na mara kinakoma kuwepo. Historia ya maisha yake inakoma. Hakipo tena.

Katika kila moja ya mafungu na mifano iliyopita, tuliona kwamba kazi hii inatimizwa kwa kusudi maalum. Inafanywa ili tuweze kupita kutoka katika hali ya kutokuwa watiifu na kuwa watiifu, kutoka katika hali ya kulalamika kuwa hatuwezi kutenda kile tunachokitamani, hadi kufikia haki ya sheria kutimizwa katika maisha yetu. Hivyo katika *Warumi* 6:6, utu wa kale unasulubishwa, mwili wa dhambi unaangamizwa, ili "tusitumikie dhambi tena."

Maumbile ni kielelezo cha ukweli wa injili kilichotolewa na Mungu. Ukweli wa fungu la sita utaonekana kwa uzito zaidi iwapo tutaweka mti wa miiba badala ya utu wa kale, na kisha ulisome fungu hilo kama litakavyomhusu mtunzaji wa bustani ambaye anataka kupata matunda mazuri badala ya miiba. Anaung'oa mti wa miiba na kupanda mche wa tufaha badala yake. Kisha anasema:

"Tukijua neno hili, ya kuwa mti wa kale umeng'olewa mpaka mizizi ili kwamba mti wa miiba uweze kuangamizwa, usizae miiba tena." Hatuna ugumu wowote katika kuona jinsi kanuni hii inavyofanya kazi katika maumbile. Tunapoitumia kanuni hii katika ulimwengu wa kiroho, tutaielewa kazi ya utakaso wa roho kwa uwazi ule ule kama hatua ya muhimu katika kupata ushindi dhidi ya dhambi.

**Ukombozi**

Sasa tumelitazama tatizo la utumwa wa dhambi, na kuona kwamba hatua ya kwanza kuelekea uhuru ni kifo cha utu wa kale. Tumeona pia kwamba kile tunachotenda ni matokeo ya jinsi tulivyo, na si kwa sababu ya udhaifu wa nia zetu. Kwa kadri sheria ya dhambi na mauti inavyodumu kuishi ndani yetu, tupo katika utawala wa nguvu za uovu ambazo huulazimisha mwili wetu wa kibinadamu kutimiza mapenzi yake, bila kujali maarifa yetu, mapenzi yetu, au dhamiri zetu zikoje.

Kwa hiyo, ili kukombolewa kutoka katika uwezo huu wa uovu ulio ndani, lazima turuhusu utolewe nje na mbali kutoka kwetu, na uhai mpya uwekwe mahali pake. Hakuna njia nyingine ya kupata uzoefu wa kuzaliwa upya. Hakuna njia nyingine ya kupita kutoka katika utumwa wa *Warumi* saba hadi uhuru wa *Warumi* nane.

Wakati utambuzi huu ni wa muhimu katika kupata ukombozi, swali linapaswa kujibiwa kwamba ni jinsi gani tunapita kutoka katika utumwa hadi ukombozi.

Ninakumbuka vizuri wakati fulani nilifundisha somo hili kwa familia moja kwa mara ya kwanza. Nililielezea tatizo kwa makini, kama ambavyo tumefanya mpaka hapa katika kijitabu hiki. Baada ya awamu hii ya somo tulisimama kidogo kwa mapumziko.

Mke alisema, "Unajua, tulisikia hubiri kama hili wiki chache zilizopita."

"Ndiyo, tulisikia," alisema mume. "Mhubiri aliliweka wazi tatizo kama ulivyofanya hapa. Kuanzia mwanzo mpaka mwisho nilisikiliza, kwani nilihitaji kulielewa tatizo na suluhisho lake. Nilijua kuwa uzoefu wangu ulikuwa kama wa Paulo katika *Warumi* saba, na nilihitaji kukombolewa kutoka kwake. Lakini wakati mhubiri alipomaliza kulielezea tatizo, alikaa chini. Katika fadhaa yangu ya kutaka kujua majibu ambayo hajayatoa, nilisimama na kusema, 'Mchungaji, umetufahamisha tatizo. Sasa tafadhali tuelezee suluhisho. Tuelezee jinsi ya kukombolewa kutoka katika nguvu hii.'

"Kwa hili mchungaji alisimama tena, kwa huzuni kubwa alisema, 'Samahani. Siwezi kuwaambia, kwani mwenyewe bado sijapata jibu lake.' Nilivunjika moyo sana kiasi kwamba sikuweza kusema neno lingine zaidi na nikarudi kukaa kwenye kiti changu kwa huzuni."

Kwa muda mwanamume yule alikaa akikumbuka juu ya uzoefu ule. Kisha akanigeukia mimi na kusema, "Je, utatufahamisha tu tatizo na kutuacha bila suluhisho lake?"

Nilifurahi sana kumwambia kwamba tunapumzika tu kwa muda, na kwamba suluhisho litafuata kwa maneno ya wazi kabisa.

Kwa namna hiyo hiyo, hatutakomea hapo. Tutalielezea suluhisho kwa kinagaubaga na kwa njia ya utendaji ulio wazi.

Kuliweka katika maneno machache, suluhisho ni injili. Huu ni uweza wa Mungu kuokoa kutoka katika dhambi.

Unaweza kuuliza kwamba, kwa nini haujaokolewa kutoka katika dhambi iwapo injili ni uweza wenyewe wa Mungu uliotolewa kukukomboa. Jibu ni kwamba, injili si uweza wa Mungu kumwokoa kila mtu.



Tukisoma *Warumi* 1:16 kwa makini, tutaliona hili. Paulo hakusema tu: "Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila" mtu. Wakati ambapo ameyatumia maneno haya katika mpangilio huo huo, hakukomea hapo. Kile alichosema kwa hakika ni kwamba, injili ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa "kila aaminiye." Maneno haya mawili zaidi yanaleta tofauti yote. Injili ni maneno mengi tu mazuri kwa asiyeamini, lakini kwa anayeamini, ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kutoka katika dhambi.

Mtume Yohana anatoa mwangwi wa ukweli huo huo katika maneno yafuatayo, "na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." *1Yohana* 5:4.

**"Utafika mpaka hapa, lakini hutapita, na hapa mawimbi yako yanyetayo [au yajivunayo] yatazuiliwa." *Ayubu* 38:11. Vivyo hivyo, kupitia neno lake Mungu ameweka kikomo cha dhambi. Ameahidi maisha ya ushindi mkamilifu.**

## Imani

Jiulize mwenyewe, "Je, ninayo imani?" Unaweza kujibu kwa haraka kwamba unahisi kwa hakika kwamba unayo imani. Unayo imani kwamba Biblia ni Neno la Mungu; una imani kwa Mungu mwenyewe kama mwenye mamlaka ya juu; una imani kuamini kwamba dhambi itapata adhabu yake; na kwamba wokovu unaweza tu kupatikana katika Yesu. Unaweza kuwa na imani katika vitu hivi vyote, lakini je, unayo imani kuishikilia injili kama uweza hai wa Mungu kukuokoa kutoka katika dhambi, yaani kukuokoa kutoka katika mzunguko wa kusikitisha wa kutenda dhambi na kuungama, kutenda dhambi na kuungama, tena na tena?

Ni sahihi kusema kwamba yeyote ambaye bado yuko katika uzoefu unaoelezwa katika *Warumi* saba, hana imani ambayo ni kushinda kuushindako ulimwengu. Imani haileti tu ushindi. Imani ni ushindi. Kwa hiyo, iwapo unayo imani ambayo Paulo anaizungumzia katika kitabu cha *Warumi*, na ambayo Yohana anaizungumzia katika waraka wake, ni hakika kwamba hautakuwa katika uzoefu wa *Warumi* saba, bali katika ukombozi wa *Warumi* nane.

Ni imani hii ndiyo ambayo Yesu aliizungumzia aliposema, "Walakini, atakapokuja Mwana wa Adamu, je! ataiona imani duniani?" *Luka* 18:8. Imani hai iletayo ukombozi kutoka katika utumwa wa dhambi haipatikani kirahisi duniani leo. Yesu alijua itakuwa hivi, na ni kwa sababu hii kwamba aliuliza swali hili. Lilimaanisha kwamba hategemei kukuta imani tele inayookoa, wakati wa kuja kwake mara ya pili.

Bado pasipo imani hii, ushindi hauwezekani. Kwa hiyo, tunahitaji kujifunza jinsi ya kuifanyia kazi imani hii. Hii imewekwa wazi katika kisa cha diwani aliyekuja kwa Yesu kutoka Kapernaumu kumwomba amponye mwanawe.

"Basi alifika tena Kana ya Galilaya, hapo alipoyafanya yale maji kuwa divai. Na palikuwa na diwani mmoja ambaye mwanawe hawezi huko Kapernaumu. Huyo aliposikia ya kwamba Yesu amekuja kutoka uyahudi mpaka Galilaya, alimwendea, akamsihi ashuke na kumponya mwanawe; kwa maana alikuwa kufani. Basi Yesu akamwambia, Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa? Yule diwani akamwambia, Bwana, ushuke asijakufa mtoto wangu. Yesu akamwambia, Enenda; mwanao yu hai. Mtu yule akalisadiki lile neno aliloambiwa na Yesu, naye akashika njia. Hata alipokuwa akishuka, watumwa wake walimlaki, wakisema ya kwamba mtoto wake yu hai. Basi akawauliza habari ya saa alipoanza kuwa hajambo; nao wakamwambia, Jana, saa saba, homa ilimwacha. Basi babaye akafahamu ya kuwa ni saa ile ile aliyoambiwa na Yesu,

Mwanao yu hai. Akaamini yeye na wote wa nyumbani mwake. Hiyo ni ishara ya pili aliyoifanya Yesu, alipokuwa ametoka Uyahudi kufika Galilaya." *Yohana* 4:46–54.

Diwani alihitaji uponyaji wa kimwili kwa mwana wake, ambaye alikuwa mgonjwa sana kiasi kwamba hakutegemewa kuishi masaa mengi zaidi. Bila shaka matabibu wa kidunia, baada ya kufanya yote wanayoweza bila kumsaidia, walimwacha angojee kifo.

Ingawa kisa hiki kinaelezea namna ya kuifanyia kazi imani kuhusiana na uponyaji wa kimwili, pia ina mafundisho ya thamani kuhusiana na uponyaji kutoka katika magonjwa ya kiroho. Kwa kweli, kusudi la kina katika kazi ya Kristo ya uponyaji wa magonjwa ya kimwili lilikuwa kufunua uweza wake kuokoa kutoka katika dhambi. Katika huduma yake ya uponyaji alionesha njia ya ukombozi kutoka katika magonjwa ya kiroho. Iwapo tunamwona Kristo kama Mmoja aliye na uwezo wa kuponya ukoma, kupooza, na mengine kama hayo tu, basi tumeshindwa kusoma ujumbe halisi katika huduma yake ya uponyaji. Katika Neno la Mungu, ugonjwa ni ishara ya dhambi (tazama *Isaya* 1:4-6), na ni ishara inayofaa sana, kama ambavyo tutaona muda mfupi.

### Ugonjwa na Dhambi

Iwapo tutalinganisha kile ambacho tayari tumejifunza kuhusu tatizo la dhambi, na tatizo la ugonjwa, tutaona namna kadhaa za kufanana. Mwana aliyekuwa mgonjwa alikuwa na akili na mwili. Katika akili yake alitamani kufanya mambo fulani, lakini ugonjwa ulikuwa ni uwezo unaokaa katika mwili wake wa kibinadamu na kuutawala, ili kwamba asiweze kufanya mambo aliyotaka. Mpaka pale ambapo ugonjwa umeondolewa ndipo angeweza kutumaini kutenda mambo anayotamani sana kuyafanya. Ni picha gani bora zaidi tunayoweza kuipata ili kuelezea tatizo la dhambi, zaidi ya tatizo hili la ugonjwa?

Yule diwani alivyosafiri kutoka Kapernaumu mpaka Kana kutafuta msaada kwa Kristo, alikwenda kutafuta suluhisho kwa tatizo linalofanana na tatizo la dhambi. Alihitaji kuondolewa kwa bwana ugonjwa kutoka katika mwili wa mwanawe, kama ambavyo tunahitaji kuondolewa kwa bwana dhambi kutoka katika miili yetu.

Pasipo swali, diwani alikwenda kwa Mtu pekee ambaye angeweza kumsaidia, na huyo alikuwa ni Yesu. Alifika na kuomba kile kile ambacho Bwana alitamani yeye awe nacho. Kwa hiyo, alikuja kwa Mtu sahihi, na kuomba kitu sahihi. Basi kwa nini Yesu alikataa kujibu ombi lake? Si kwa sababu Yesu alichagua tu kufanya hivyo, wala si kwa sababu yule diwani alikuwa amevuka mpaka wa fadhila za Mungu. Sababu pekee iliyomfanya Kristo asimponye yule mvulana ilikuwa ni kwamba njia ambayo diwani alimjia ilifanya isiwezekane kwa Kristo kufanya hivyo.

Ni mara ngapi tumepiga magoti kuomba msamaha kwa ajili ya dhambi, na kumsihi Bwana atupe ushindi dhidi yake, na bado tukakuta kwamba dhambi iko pale pale kana kwamba hatujaomba kabisa? Tumekwenda katika njia yetu tukiwa na fadhaa na kutatanishwa na hili, pasipo kuelewa ni kwa nini Bwana hajajibu maombi yetu. Tulishindwa kuelewa kwamba ingawa tumeomba kile Bwana anachotamani kutupa, hatujaomba kwa imani ya kweli. Vivyo hivyo, iwapo diwani asingefika mahali akaliona kosa lake katika njia ambayo alimjia Kristo basi baada ya kurudi nyumbani angemkuta mwanawe amekufa. Lakini diwani aligundua kosa lake na kubadili njia yake, kufuatana na sayansi ya kweli ya maombi. Wakati alipokuja akiwa anaamini, ombi lake lilisikiwa na kujibiwa.

Yesu hakumwacha diwani katika hali yake ya kutojua ukosefu wake wa imani. Alimwambia kwa huzuni, "Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa?" *Yohana* 4:48. Kumwambia mtu huyu, kwamba "hamtaamini kabisa," ni kusema kwa lugha ya wazi kuliko zote, hauamini bado; wewe bado ni asiyeamini.

Lakini tusisahau ukweli kwamba diwani alijua kwamba analo hitaji kubwa. Iwapo wewe ni mwaminifu kwa nafsi yako mwenyewe, nawe pia utatambua hili. Mtu yule alijua kwamba hakuna uwezo wa kidunia ambao ungeweza kumponya mwanawe. Vivyo hivyo unajua kwamba hakuna uwezo duniani unaoweza kukuokoa kutoka katika dhambi. Mtu huyu alikuja kwa Kristo akiwa na ombi lake. Vivyo hivyo na wewe pia unakuja kwa Kristo ukiwa na ombi lako la kuokolewa kutoka katika dhambi zako. Kwa kweli, diwani alimwomba Kristo, kwani kitendo cha kuliweka hitaji mbele ya Kristo ni ombi. Kwa njia hiyo hiyo, wewe pia umemwomba Kristo.


Hata hivyo Kristo alimwambia diwani wazi wazi ya kuwa licha ya ombi lake alikuwa ni asiyeamini. Kristo hakuweza kumfanyia lolote katika hali hiyo. Vivyo hivyo, iwapo unajikuta upo katika uzoefu wa *Warumi* saba, baada ya kufanya yote unayoweza ili kupata ushindi dhidi ya dhambi zako, basi wewe pia ni asiyeamini. Na iwapo wewe ni asiyeamini, unahitaji kuelewa njia ya imani—imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa roho.


Basi ni nini ambacho hakikuwa sahihi katika njia ya kwanza ambayo kwayo diwani alimjia Yesu? Maneno ya Kristo kwake yanafunua jibu: "Msipoona ishara na maajabu hamtaamini kabisa." Kwa maneno mengine, mtu huyu alikuja kwa Yesu akiwa na ombi lake, akaliweka ombi lake mbele yake, na kisha akasubiri kuona iwapo ataweza kulitimiza. Iwapo Yesu atamponya mwanawe, basi atamwamini.

Hii siyo njia ya imani inayookoa, na kamwe haiwezi kuwa. Hata sasa iwapo kila mmoja wetu atarudia kuchunguza kwa uaminifu njia ambayo tumekuwa tukimjia Mungu katika maombi, tutagundua kwamba tumekuwa tukimjia kama diwani alivyofanya. Tumekuja kwa Bwana na kumwomba atubariki. Kisha tumekwenda zetu, tukisubiri mbaraka huo kumiminwa kwetu kabla hatujajiandaa kuamini kwamba tunao mbaraka huo. Kwa kweli, ni sahihi kusema kwamba iwapo Bwana angetupa mbaraka ambao tumemwomba, badala yake tungebaki tunashangaa kuuona.

Muda muafaka wa ukweli ulifika kwa diwani, kama vile ambavyo ni lazima ufike kwetu pia iwapo tutapata uzoefu wa imani inayookoa. Mwokozi anapotamka maneno ya kutukemea, Roho wa Mungu hutuhakikishia juu ya dhambi. Yeye huyachukua maneno hayo ndani kabisa katika dhamiri zetu na kufunua kasoro katika tabia zetu. Ndivyo ilivyokuwa kwamba maneno ya Yesu yalitosha, chini ya huduma ya Roho Mtakatifu, yalitosha kumfunulia diwani ule moyo wake wa kutokuamini. Hivyo alipoona kile Mwokozi alichomfunulia alilikubali kemeo. Aliuona uweza wa Kristo, na imani yake ilishikilia uweza huo. Tunatambua hili kwa sababu ya mwitikio wa Yesu kwa ombi lake lililofuata.

Sasa ombi la mtu huyu kwa Yesu likawa, "Bwana, ushuke asijakufa mtoto wangu!" *Yohana* 4:49. Kulikuwa na tofauti kubwa katika ombi hili. Inawezekana pasiwepo na tofauti ya wazi ya mpangilio wa maneno yenyewe, lakini tunajua kwamba kulikuwa na tofauti kutokana na mwitikio wa Yesu kwalo. Ombi la kwanza lilileta tu kemeo la kuhuzunisha, wakati la pili lilileta uponyaji. Hivyo tofauti ilikuwa ni nini? Tofauti ni kwamba sasa mtu huyu alikuwa ni mwenye imani. Tunajua hili kwa sababu Maandiko yanatuambia hivyo: "Mtu yule akalisadiki lile neno aliloambiwa na Yesu naye akashika njia." *Yohana* 4:50.




Kana haikuwa mbali sana kutoka Kapernaumu—si zaidi ya kilomita ishirini na tano. Kristo aliyatamka maneno yale kwa baba huyu, mnamo saa ya saba, kama saa saba mchana, ili kwamba baba huyu aweze kutembea kwa urahisi mchana huo kuelekea nyumbani. Lakini hakufanya hivyo. Iwapo angehitaji kuona kwa macho yake kwamba mwanawe alikuwa kweli ameponywa angeweza kufanya hivyo. Lakini tayari alijua kwamba mwanawe yu mzima. Muda mfupi kabla hajafika nyumbani siku iliyofuata, watumishi wake walimweleza kile imani

ilichomwambia siku iliyotangulia. Bila shaka walifadhaishwa na kutokuwepo kwa mshangao wowote kutoka kwa baba huyu walipomwambia kwamba mwanawe alikuwa mzima.

### Ombi la Imani

Hebu sasa tulinganishe ombi la kwanza la diwani, ambalo lilikuwa ni la kutokuamini, na ombi lake la pili, ambalo lilikuwa limejaa imani. Akiwa katika hali ya kutokuamini, aliomba na kupata maono ya uweza ulio ndani ya Mwana wa Mungu. Kadri imani yake ilivyoushikilia uweza huo, aliona ndani yake jibu kamili kwa hitaji lake. Hivyo aliomba kipawa hicho, na alikishikilia kwa imani, akijua kwamba kipawa kile kilikuwa ni chake tayari. Kisha akaenda zake akijua kwamba mbaraka, ambao tayari alikuwa nao, utadhihirika wakati atakapouhitaji zaidi.

Hatua hizi hizi zinafunua kanuni ya njia ya imani yenye mafanikio kwetu pia.

Kwanza, lazima tuwe na ufahamu sahihi wa tatizo tunalokabiliana nalo. Katika wakati uliopita umekuja kwa Mungu mara ngapi ukiomba msamaha kwa kile ulichotenda, bila kukiri tatizo halisi na kuomba kuondolewa kwa sheria hiyo ya dhambi kutoka ndani yako? Kulikuwa na ukosefu wa ufahamu wa hali halisi ya tatizo la dhambi. Huu ni upungufu mkubwa ambao lazima ujazwe kabla hatujaweza kuomba kwa ufahamu na kwa mafanikio.

Pili, lazima tuzijue ahadi za Mungu mpaka ziwe si tu maneno yaliyo katika Biblia, bali uweza halisi wa Mungu ukizungumza nasi. Ili kufanya hivi, tunahitaji kujifunza ahadi hizo mpaka zizame katika fikra zetu na kuwa sehemu yetu.

Tunapaswa kuchunguza na kujifunza ahadi kuu za Biblia zinazohusu ushindi binafsi dhidi ya dhambi, ili kwamba tuzijue toka moyoni. Iwapo tunataka kuwa washindi na pia kuuhifadhi huo ushindi binafsi juu ya dhambi, lazima ahadi hizi ziwe sehemu yetu hai. Zinatakiwa ziwe pale, tayari kububujika toka mdomoni katika kujibu mashambulizi yoyote ya adui, au pendekezo lolote kutilia mashaka uweza wa Mungu kuokoa kutoka katika dhambi.

Ahadi kuu katika Biblia ni nyingi kama jinsi zilivyo na uwezo utendao kazi kuokoa kutoka katika sheria ya dhambi na mauti. Kila mmoja wetu anapaswa kuzitafuta mwenyewe. Ifuatayo ni mifano michache kwa wale wanaotaka kuanza kujikusanyia ahadi hizi za ushindi dhidi ya dhambi.

"Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi." *Warumi* 6:14. Jifunze maneno haya mpaka utambue kwamba yenyewe ni ahadi ya Mungu kwako binafsi, kwamba dhambi haitakutawala, wala kuwa na uwezo juu yako.

"Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili." *1Wakorintho* 10:13. Kama ambavyo wazazi hawawezi kuruhusu mtoto akabiliane na hatari ambayo ni kubwa kuliko umri wake wa utoto, vivyo hivyo Bwana hataruhusu jaribu ambalo ni kubwa kuliko uwezo wako kukujia. Kwa kila jaribu linalokuja kwako, Yeye ameandaa njia ya ukombozi. Wakati uweza huu mkubwa mno umetolewa kwa wokovu wa kila mtu, basi itawezekanaje kuwepo na udhuru kwa dhambi katika maisha ya mtu yeyote? Tunaweza "kuyafanya mambo yote katika Yeye" atutiaye nguvu. *Wafilipi* 4:13.

Hapa kuna nukuu zaidi: *Mathayo* 1:21; *Yohana* 8:36; *1Wakorintho* 15:34; *1Wakorintho* 15:57; *2Wakorintho* 2:14; *Wafilipi* 1:6; *1Wathesalonike* 4:3; *1Wathesalonike* 5:23, 24; *1Petro* 1:5; *Yuda* 24; Katika Agano la Kale, *Zaburi* 23 na 46 hasa ni ahadi nzuri za uwezo kwa ajili ya ukombozi. Jipatie pia uwezo ulio katika *Ezekieli* 11:19, 20; na *Ezekieli* 36:26.

Kusudi kubwa katika kuzijua ahadi ni ili kuijenga imani—imani itakayofanya kazi ya kuitakasa nafsi. Kadri ahadi hizi zinavyosomwa na kusomwa zaidi na kufanywa kuwa sehemu yako, ndivyo zitakavyoijenga imani yako zaidi. Hatimaye, wakati utafika ambapo utajikuta ukiushikilia uweza, na kupata ukombozi ambao imani pekee inaweza kuuleta. Imani hai katika uweza wa Mungu unaookoa siyo kitu kinachoibuka na kukua chenyewe ndani yetu. Siyo kitu tunachoweza kukizalisha ndani yetu sisi wenyewe. Hii haiwezekani. "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa Neno la Kristo." *Warumi* 10:17.

Wakati tunapofika katika hatua ambapo imani hai imeshikilia na kuamini ahadi za Mungu, basi ni wakati wa kuchukua hatua ya tatu. Hii ni kuja kwa Kristo na kuomba mbaraka. Usiombe lile ombi la kale ambalo limeshindwa kukuletea mafanikio kwa muda mrefu.

Wakati uliopita mtindo wa maombi umekuwa, "Bwana, nimetenda dhambi. Tafadhali nisamehe kwa hicho ambacho nimekitenda." Unaweza ukawa umeahidi kutotenda dhambi

hiyo tena, au kuomba msaada ili usiitende tena. Njia hii haijakuletea ushindi wakati uliopita na pia haitaweza kwa wakati ujao. Lazima kuwepo na badiliko, kama vile diwani alivyolazimika kubadili njia yake kuja kwa Kristo.

Unahitaji kuomba katika mfumo ufuatao: "Bwana, nimefika mahali ambapo ninaona kwamba tatizo halisi ni asili ovu iliyomo ndani yangu. Nayo ni 'uwezo wa dhambi,' 'sheria ya dhambi na mauti,' 'mwili wa mauti,' 'nia ya mwili,' na 'moyo wa jiwe.' Wakati huo ungali pale, mimi ni mti mwovu na ninaweza tu kuzaa matunda maovu, kwani mwili wangu upo chini ya utawala wa uwezo huo. Bwana, umeahidi kuondoa moyo wa jiwe na kunipa moyo mpya kabisa. Ninaamini kwa hakika kwamba utafanya hili, na kwa hiyo ninakupa moyo huu wa kale. Uondoe kutoka kwangu. Siutaki. Weka moyo mpya mahala pake na unifanye niwe mshiriki wa asili yako ya uungu. Kwa imani, na hivyo kwa kweli, ninapokea kipawa hiki chenye heri na ninakushukuru kwacho. Kwa jina la Yesu linalookoa, Amina."

Iwapo unayo imani hai, basi hautasubiri kuuona mbaraka kabla haujafahamu kwamba unao. Wakati huo utajua kwamba umekombolewa, kwamba dhambi haikutawali tena juu yako, na kwamba umekuwa mtoto wa kweli wa Mungu hatimaye. Kwa kweli, itakuwa bado ni lazima kuupinga mwelekeo wa kawaida wa kibinadamu wa kusubiri kuona matokeo kabla haujaamini. Usitarajie kuona kwamba umebadilishwa. Amini tu hivyo kwa sababu Neno la Mungu linasema hivyo, na muda mfupi sana utagundua kwamba hivyo ndivyo ilivyo.

Diwani hakusubiri kumwona mtoto wake akiwa hai na mwenye afya kabla hajaamini kwamba alikuwa ameponywa kabisa. Hakuhitaji kuona, kwani alikuwa na Neno la Mungu kupitia kwa Kristo kwamba ilikuwa hivyo na hilo lilitosha. Imani hutegemea Neno la Mungu, siyo katika kuona kwa macho na hisia, ambazo zinaweza kubadilika haraka sana. Kwa hiyo, ili kuelewa uhusiano wetu na Mungu, tunapaswa kuangalia katika Neno la Mungu na kuruhusu hilo, liwe kiongozi wetu, badala ya hisia zetu.

### Ushuhuda Binafsi

Mtume Yohana anasema, "Hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi pia mpate kushirikiana nasi." *1Yohana* 1:3. Wale wanaoweza kuwasaidia wanadamu wenzao kwa ubora zaidi ni wale wanaoweza kushuhudia kutoka katika uzoefu wao wenyewe. Wanaweza kusema kile wanachokijua, badala ya nadharia tupu. Kama uhakikisho kwa wengine, kwamba hii ni njia ya mafanikio iliyojaribiwa na kuthibitishwa, nitaeleza jinsi ambavyo imefanya kazi katika maisha yangu. Wapo watu wengine wengi duniani ambao wamesikia ujumbe huu na wanaweza vile vile kushuhudia ushindi dhidi ya dhambi katika maisha yao pia.



**Mwonekano wa dunia kutoka angani. Mwanadamu amepata ushindi mkubwa dhidi ya mazingira yake, lakini ushindi halisi ambao anahitaji kuupata ni ushindi dhidi ya nafsi yake.**

Zamani katika mwaka 1953, nalijiunga na wafanyakazi wa chuo cha kimisionari kama mwalimu. Mwaka uliofuata nilichaguliwa kuwa mzee wa kanisa. Nililipenda kanisa na nilijihusisha kwa kweli katika shughuli zake. Niliyaelewa na kuyaenda mafundisho na kuyahubiri kwa bidii na shauku. Niliamini kuwa nilikuwa na uhakika wa wokovu kama ambavyo yeyote angekuwa, na siku baada ya siku nilitulia katika tumaini la uzima wa milele.

Maisha yangu yalionekana kuwa "mazuri" kwa nje, lakini kwa ndani nilikuwa na matatizo ambayo sikuweza kupata ushindi dhidi yake. Nilikuwa ni mwalimu wa useremala na ilionekana kwamba wavulana ambao hawakufaulu katika masomo ya nadharia walikuwa wakiletwa kwenye darasa langu. Wengi wa vijana hawa walikuwa wamekuza upinzani mkubwa katika kujifunza kiasi kwamba darasa likawa ni mahali pa mapambano ya kila siku kati ya juhudi zangu kuwafundisha, na juhudi zao kupinga kujifunza.

Nilijikuta kwamba uvumilivu wangu ukijaribiwa kupita mipaka yake, nikawa na hasira dhidi yao. Kulikuwa na nyakati ambapo kwa furaha, ningeweza kuwagongeza vichwa vyao ukutani. Lakini kulikuwa na mvuto uliokuwa ukinizuia kufanya hivyo. Nilikuwa na sifa njema ya kulinda. Sikutaka kukaripiwa na mkuu au bodi ya chuo, hivyo nilificha ghadhabu yangu na kuidhibiti kiasi kwamba haikuwahi kijionesha kwa nje.

Iwapo ukichukua bwela ya mvuke na kuwasha moto chini yake, huku matundu yake yote yakiwa yamefungwa, itastahimili kwa muda. Lakini presha itaendelea kupanda zaidi na zaidi. Ikiwa moto utazimwa kwa muda presha itapungua bila kuwepo na mlipuko kwa kishindo, lakini moto ukichochewa tena, muda utafika ambapo bwela hiyo italipuka. Kadri muda ambao bwela inastahimili presha inayoongezeka unavyokuwa mwingi, ndivyo mlipuko wake huwa mkubwa zaidi hatimaye.

Ndivyo ilivyokuwa kwangu. Kadri presha ya jaribu dhidi yangu katikati ya wiki ilivyochochea joto hasira yangu siku baada ya siku, nilifunga matundu yote ili kwamba hasira iliyo ndani yangu isiweze kutoka. Lakini ilikuwemo ndani yangu hata hivyo, na wakati ulikuwa unakuja ambapo italipuka. Kadri nilivyovumilia kwa muda, ndivyo mlipuko ulivyokuwa mbaya zaidi wakati ulipokuja hatimaye. Kwa kawaida ulitokea mwishoni mwa wiki nikiwa nyumbani. Kwa kawaida mke wangu na watoto wangu wasiostahili wakawa ndiyo wapokeaji wa ghadhabu ambayo wengine waliizalisha.

Wakati maneno yote makali yalipokuwa yamekwisha kunenwa, na presha yote iliyokuwa imefungwa ilipotoka, basi nilijisikia mwenye hatia na majuto. Nilikwenda kwa Bwana na kuomba msamaha wake na kuahidi kwa dhati kabisa kwamba nisingetenda hivyo tena. Kwa nia thabiti, na yenye ujasiri nilirejea darasani, na kukuta utaratibu ule ule ukijirudia. Tena, mtazamo wa wale vijana uliamsha hasira yangu. Tena, nilifunga matundu yote. Tena, kulikuwepo na ongezeko polepole la hasira na mlipuko. Tena, kulikuwepo na toba na ombi kwa ajili ya msamaha. Kisha hili bado lilifuatwa na kushindwa kwingine.

Nilikuwa ninajaribu na kushindwa, kutenda dhambi na kutubu, kutenda dhambi na kutubu, tena na tena. Huu ulikuwa ni uzoefu wa *Warumi* saba bila shaka. Sikuweza kujielewa mwenyewe na kitabu cha *Warumi* kilionekana kuwa kigumu kueleweka kuliko vitabu vyote katika Biblia. Nilichunguza ili kupata jibu. Nilisikiliza wahubiri wengine ili kuona ni nini wanachoweza kusema kuhusiana na suala hili, lakini pote ilikuwa wazi kwamba hata viongozi wenye uwezo zaidi kanisani walikuwa wanapitia uzoefu ule ule wa kukatisha tamaa kama nilivyokuwa mimi.

Hivyo nilitulia katika falsafa ya kujilinda ambayo ilielezea kwa kibinadamu kuwa tabia yangu ni uzoefu wa kawaida ya wale wanaookolewa. Nilihoji kwamba nilikuwa na bidii na mwaminifu, kwamba nilikuwa ninafanya kwa kadri nilivyoweza, na kwamba katika siku kuu ya hukumu Mwokozi atasema, "Mtu huyu alifanya kwa kadri alivyoweza, ingawa aliishi maisha ya dhambi duniani. Hivyo tutamsamehe na kumpa nafasi katika ufalme."

Kisha ilifika siku nilipokutana na kijana mmoja ambaye kwa kweli alikuwa amejazwa na joto la uzoefu mpya wa ukombozi. Hakuwa na kitu kingine alichotaka kuzungumzia zaidi ya hiki. Mwanzoni maongezi yake nami yalionekana kama lugha ya kigeni, kwani alikuwa akizungumzia uzoefu na maisha niliyokuwa siyajui.

Kisha kwa ghafla aliniambia. "Je, unajua ina maana gani kuwa na ushindi kila siku dhidi ya kila dhambi inayofahamika?" aliuliza.

Katika kujibu nilicheka. "Kwa nini," nilimwambia kwa mshangao, "kwa miaka kumi kamili nimekuwa nikiutafuta uzoefu kama huo. Hakuna hata mmoja ambaye ameomba kwa dhati au kujaribu kwa bidii zaidi ya jinsi ambavyo nimefanya kuupata. Sijakutana na mtu yeyote aliye nao. Tazama, ninajaribu kila siku kwa kadri ninavyoweza. Mwishoni mwa siku ninaomba msamaha wa dhambi zangu. Ninaamini kwamba Mungu ananisamehe, na katika siku ya ufufuo, Mungu ataikubali tabia yangu kama kitu bora nilichoweza kufanya, na ninaamini kwamba nitaokolewa."

Kamwe sitausahau mwitikio wake. Ulikuwa si wa maneno bali ulionekana usoni. Uso wake ulisema kwa wazi, "Ndugu unahitaji msaada, tena unauhitaji sana na haraka." Ujumbe huo wa kimya ulifanya mvuto mkubwa kwangu kiasi kwamba wakati aliponiuliza iwapo anaweza kuja na kunipa somo la Biblia juu ya suala hilo nilikuwa mwepesi kupanga.

Ninadhani kwamba sikuwahi kupewa somo geni kama hilo. Alikuwa akisoma fungu la maandiko. Kisha alifanya juhudi kutoa maoni yake na kulielezea, lakini alionekana kuishiwa

na maneno na hivyo kugeukia fungu lingine ili kujiokoa mwenyewe. Kwa namna hii somo liliendelea, na halikuleta chochote zaidi ya kusoma fungu moja baada ya lingine. Kwa uaminifu niliyanukuu yote kwenye kipande cha karatasi.

Baada ya kumaliza nilibishana naye kwa kutumia hoja zangu zote nilizoweza kuzifikiria, na kisha nilimtazama akiondoka. Lazima aliondoka akiwa anajisikia kukatishwa tamaa kabisa, akiwa ameshawishika kwamba nilikuwa mwanafunzi nisiyefaa kwa ujumbe wake wa ukombozi.

Siku kadhaa zilipita wakati ambapo uwezo wa maandiko yale ulifanya kazi katika akili yangu. Hapakuwa na chochote kilichokuwa wazi au kuelezeka vema. Hii ilinikumbusha yule mtu kipofu ambaye alianza kuona. "Akatazama juu, akasema, 'Naona watu kama miti inakwenda.'" *Marko* 8:24.

Siku nne zilipita. Ilikuwa ni siku ya Jumatano mchana na nilirudi nyumbani kwa muda mfupi wakati wa mapumziko, na kukaa chini nikiwa na orodha ile ya mafungu. Nikaanza kuyasoma tena moja baada ya lingine. "Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi." *Warumi* 6:14. "Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." *1Wakorintho* 15:57. "Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae." *Yuda* 1:24.

Kadri nilivyosoma kila fungu, nilifanya hivyo kwa kutafakari na taratibu, nikiruhusu maana yake izame katika akili yangu na Roho Mtakatifu alililifafanua Neno la Kweli. Niliendelea chini mpaka nikamaliza theluthi moja ya mafungu kwenye orodha ile, ndipo ghafla uhakikisho mkubwa ulikuja juu yangu. Mpaka hatua hii nilikuwa ninaamini kwamba siwezi kuishi bila dhambi. Ghafla maana halisi ya kutisha ya imani hii ilinijia katika akili yangu kwa msukumo mkubwa. Niliona kwamba, kuamini kuwa nitatenda dhambi kila siku, ilikuwa ni kuamini kwamba Shetani ni mwenye uwezo zaidi ya Kristo, na kwamba dhambi ilikuwa na nguvu kuliko haki. Mara tu nilipoelewa ukweli huu, niliona kwamba maisha yangu yalikuwa hayajashuhudia uwezo wa Mungu bali uwezo wa Shetani. Hali ambayo ilifanya ushuhuda huo useme zaidi sana kuutetea upande wa Shetani ilikuwa ni ule ukweli kwamba niliushikilia msimamo huo na kudumisha ungamo nililolifanya.

Sasa Roho wa Mungu kwa hakika aliweza kufanya kazi ndani yangu kwa hakika. Niliona yote niliyoyatumainia kama ushahidi kwamba nilikuwa mtoto wa Mungu yakifagiliwa mbali nami—ujuzi wangu, juhudi zangu, madaraka yangu, na upendo wangu kwa ukweli kama nilivyouelewa. Vyote hivi sasa havikunipatia dhamana yoyote. Nilijiona mwenyewe kama Mungu alivyoniona—nisiye na tumaini, niliyepotea, niliyehukumiwa milele. Nilikumbwa na giza la kukata tamaa kwa namna ya kutisha; giza la utambuzi wa kutisha kwamba sitatokea katika ufufuo wa wenye haki. Katika maisha yangu yote, sijawahi kuona wakati ulio na giza au wa kutisha zaidi ya huo.

Kwa namna fulani, na mpaka leo hii sijui ni kwa namna gani, Bwana alinipa uaminifu wa wazi kukubali kwamba haya yote yalikuwa ni kweli kabisa. Sikurudi nyuma tena na kuukanusha ukweli huu kwa kusema kwamba nilikuwa mzee wa kanisa, mwalimu wa chuo, mtu niliye na ujuzi mzuri wa Maandiko, mhubiri, mtu mwenye sifa njema, mwenye juhudi na ari ya kujitoa nafsi kwa ajili ya ukweli. Ninamshukuru Bwana kwa hili, na ninaomba kwamba wakati wa kutisha wa kujua ukweli utakapokujia, utakubaliana nao na kuupokea kama ulivyo. Iwapo utauzima uhakikisho ambao Roho Mtakatifu anauleta, mwishoni utafunga mlango dhidi ya kazi ya neema inayofanywa kwa ajili yako, na hiyo itakuwa ni hasara ya milele.

Bwana hajeruhi tu bali ili aponye. Katika wakati huo huo ambao nilijiona kama mwenye dhambi aliyepotea bila tumaini na kuukubali ukweli huo, Bwana alizifunua ahadi katika ufahamu wangu kwa namna ambayo sijawahi kuziona hapo awali. Ilikuwa kama vile zilikuwa zimeandikwa kwa ajili yangu binafsi. Imani hai ilichipuka katika moyo wangu kadri nilivyoona uwezo katika Neno la Mungu. Nilianguka pembeni ya kiti na kuomba kwa mara ya kwanza katika maisha yangu: "Bwana, sasa ninaona kwamba tatizo siyo kile ambacho nimetenda, bali ni jinsi nilivyo. Uhai huu mwovu ndani yangu ndio chanzo cha tatizo. Kama ugonjwa, uhai huu ndiyo bwana wa mwili wangu, hivyo siwezi kufanya mambo ninayotaka kufanya na ninajua kwamba ninapaswa kuyafanya. Huu hapa uhai wangu wa kale; utwae na unipe uhai wako mpya badala yake. Bwana, ninakushukuru kwa huo, katika jina la Yesu linalookoa, Amina."

Niliinuka kutoka katika magoti yangu. Katika utu wangu wote nilitambua kwamba nimezaliwa mara ya pili. Haikuwa ni hisia, kwani sikuhisi tofauti yoyote. Ulikuwa ni uhakikisho. Ulikuwa ni ushahidi wa imani iliyojikita katika Neno la Mungu. Ulikuwa ni

utambuzi huo huo ambao ulimwongoza diwani kufanya safari yake ya kurejea nyumbani taratibu sana, kwani alijua kwamba mtoto wake alikuwa amepona. Hapakuwa na haja kwake kuharakisha kurudi nyumbani kuona iwapo ilikuwa hivyo. Tayari alijua, vivyo hivyo na mimi. Ushuhuda wa macho unaoonekana ungekuja baadaye, kama ilivyofanyika kwa diwani.

Katika siku hizo tulimiliki gari Muundo wa A Ford. Mara nyingi mke wangu aliiendesha kwenda mjini, lakini si nyakati zote aliweza kufanikiwa kurejea tena. Kulikuwepo na nyakati ambapo nilipokea simu kutoka kwake akisema kwamba amekwama. Nyakati zingine kuacha kazi yangu na kwenda kumsaidia ilikuwa ni usumbufu sana, na nilikuwa nikikerwa sana kuhusu hilo. Kwa maneno ya hasira na kukosa subira nilimwambia hivyo pia. Kupitia matatizo haya yote, ndoa yetu ilielekea kuharibika. Baada ya haya yote kumalizika, ningejisikia vibaya kuhusu tabia yangu na ningeungama na kudhamiria kwamba haitatendeka tena. Ninakumbuka siku ambapo simu iliita kwa mara nyingine tena na nilijikumbusha kwamba nilikuwa nimedhamiria kuwa mwenye subira na upendo. Yote yalikwenda vizuri kwa dakika chache. Kisha spana iliteleza. Nilijichubua mkono. Hasira ilipanda na muda mfupi ulifuatiwa na mbubujiko wa maneno tena. Hisia za huzuni za "Inanifaidia nini" zilinijia. Niliendesha kuelekea nyumbani, nikiwa kimya na mwenye kushindwa nikiwa siwezi kujielewa mwenyewe.

Wakati siku yangu ya ukombozi ilipofika, sikujisikia tofauti yoyote ndani yangu. Hapakuwa na presha zozote maalumu kwangu wakati huo. Moto wa bwela ulikuwa umezimika, ulikuwa ni wakati wa likizo na niliishi maisha ya furaha kabisa kutoka siku hadi siku. Kisha ikafika Ijumaa mchana ambapo kwa mara nyingine mke wangu aliichukua gari na kutoka nayo na nilipokea simu kwa ajili ya msaada kutoka mjini kilometa nne hivi.

Bila kutoa nafasi kwa wazo la pili kuhusu jinsi ninavyopaswa kutenda, nilikwenda kwake kwa haraka kadri inavyowezekana na kuitengeneza gari. Kwa kuwa sikuweza kuiwasha nilimruhusu aende nyumbani pamoja na jirani ambaye kwa bahati alipita karibu. Mwishoni nilifanya mpango wa kuivuta gari na kuirejesha. Kisha nilikwenda nyumbani kwa ajili ya chakula cha jioni. Baadaye tulihudhuria ibada ya jioni kanisani na kisha kurejea nyumbani kwa pumziko la usiku.

Nilikuwa karibu kabisa kupata usingizi. Mke wangu alikuwa amelala kimya kabisa pembeni yangu, akiwa katika mawazo mazito. Sikumjali sana mpaka aliponiuliza ghafla, "Nini kimetokea kwako?"

Sikuwa na wazo hata kidogo juu ya kile alichokuwa anakizungumzia na hivyo nikamsihi anieleze alikuwa anamaanisha nini. Kwa kujibu, alisema, "Kitu fulani kimetokea kwako na ninataka kujua ni nini." Nilimwambia tena kwamba sikujua ni nini anachokizungumzia na nikaomba maelezo.

"Alasiri ya leo nilisubiri kwenye gari nikitarajia mashtaka ya kawaida ya hasira wakati ulipofika. Lakini badala yake, ulifanya tu kile ulichoweza na kisha ukaniruhusu niende nyumbani. Nilifurahi kuondoka pale, lakini nilijiambia kuwa wakati utakapofika nyumbani ndipo nitayapata. Lakini ulipofika bado haukusema chochote. Hivyo nilidhani, hayo yatakuja baada ya chakula cha jioni. Tena ulienda zako, kwa utulivu na amani. Hatimaye nilifikia hitimisho kwamba umeyazuia hayo vizuri kwa wakati huu, lakini utakaporudi nyumbani ukiwa umechoka baada ya kumalizika kwa mkutano na tutakapoingia kulala kitandani, hayo yangekuja. Lakini bado hayajaja, hata sasa. Kitu fulani kimetokea kwako na ninataka kujua ni nini."

Ilikuwa ni wakati ule ndipo ushahidi unaoonekana wa badiliko kuu ambalo lilitokea ndani ulikuwa mbele yangu. Ghafla nilitambua kwamba katika utendaji wote, nilitenda kwa mujibu wa jinsi nilivyokuwa sasa, vile vile kama hapo zamani nilivyotenda kama nilivyokuwa. Wakati ambapo hapo awali, mwitikio wangu wa asili ulikuwa ni ule wa kukosa subira na kupandwa na hasira, sasa ulikuwa ni ule wa amani na subira. Mshangao wa yote haya ulinijaa kiasi kwamba nilijikuta siwezi kujibu, wakati katika moyo wangu kuliibuka ushuhuda wa moyo, "Neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu." *Zaburi* 118:23.

Wewe pia, utakapofika mahali ukapata badiliko hili la ajabu ndani, na kuona utendaji wake mpya kabisa na kuchukuliana na mashinikizo ya maisha kwa njia nyingine, ndipo utajua na kuelewa vile nilivyojisikia katika muda huo. Ulikuwa ni uzoefu wa ajabu na wenye heri kabisa.

Kwa miaka yote arobaini iliyofuata uweza wa ukweli huu umejaribiwa katika uwanja wa mapambano wa maisha yangu. Japokuwa, siwezi kushuhudia kwamba sikuwahi kutenda dhambi katika muda huo, lakini ninafurahi kwamba ninaweza kushuhudia ukweli wa thamani kwamba ujumbe huo bado unatenda kazi katika maisha yangu vile vile kama ulivyofanya

nilipopata uzoefu wake mara ya kwanza. Wakati ambapo nimetenda dhambi mara zote imekuwa ni upungufu wangu—nilikosa imani, au sikuwa makini kudumusha muunganiko wangu na Mungu, au mengine kama hayo. Haijawahi kuwa kwa sababu ya upungufu wa uweza wa injili.

Maisha yamekuwa tofauti sana tangu siku hizo za kushindwa. Hapo awali ilikuwa marudio ya kudumu ya mapambano yale yale dhidi ya dhambi zile zile, bila kufanikiwa kutoka kwenye mzunguko wa kutenda dhambi na kuungama tatizo lile lile mwaka hadi mwaka. Mzunguko huo wa kukatisha tamaa uliachwa nyuma wakati kazi ya ushindi iliposonga mbele kwenye maeneo mapya kadri nuru zaidi na zaidi ilipokuja. Kitabu cha *Warumi* hakikuwa siri tena kwangu. Kikawa ni furaha kwangu kukisoma, kwani sasa niliweza kuelewa kile Paulo alichokuwa anakisema.

Sehemu ya 3

# Baada ya Kuzaliwa Upya

### Si Kutoka Utumwa Hadi Utumwa

Mara baada ya kuwa tumezaliwa upya, mfuatano mpya wa mambo huanza. Kwa kweli, kuzaliwa upya siyo mwisho wa njia bali ni mwanzo wa maisha mapya. Tunasisitiza suala hili kwa sababu kuna hatari halisi ya kutoelewa kile ambacho kwa kweli kinatokea wakati wa kuzaliwa upya. Ni kweli kwamba asili ya kale imeondolewa na asili mpya imechukua nafasi yake. Lakini je, hii ina maana kwamba mara tunapozaliwa upya hatuwezi kutenda dhambi tena?

La, haimaanishi kitu chochote kama hicho. Hatupiti kutoka aina moja ya utumwa na kwenda katika aina nyingine ya utumwa, bali kutoka katika utumwa hadi uhuru. Tunapokuwa chini ya utawala wa ile asili ovu, tunalazimishwa kutenda dhambi, lakini baada ya kuwa Wakristo wa kweli tunakuwa na uchaguzi wa kumfuata Kristo au Shetani. Uchunguzi mfupi wa tofauti kati ya mabwana hawa wawili utaliweka hili wazi.

Wakati tunapokuwa katika hali ya *Warumi* saba, tuna ile nia ya mwili ndani yetu, ambayo ni bwana aliye dikteta, ambaye uwezo wake unauzidi sana ule wa nia zetu wenyewe. Huyu bwana huitawala nia ili kuzitumikia tamaa zote za mwili wa kibinadamu ulio wa dhambi na kuutumia huo mwili kama silaha ya udhalimu. Ukweli huu unaelezwa katika mchoro ufuatao

**MTU WA WARUMI SABA**

**Nia ya mwili:**

Bwana katili, dikteta ambaye hubatilisha uamuzi wa nia ili kuutawala mwili wa kibinadamu ulio dhaifu, ulioanguka, wa dhambi.



**MTU WA WARUMI NANE**



**Nia ya uungu:**

Uweza ambao ushirikiana na nia ili utiisha mwili huo huo a kibinadamu, ulio haifu, ulioanguka, wa dhambi.

Baada ya sisi kuzaliwa upya na kuingia katika uzoefu ulioelezwa katika *Warumi* nane, tunakuwa hatuna nia ya mwili tena. Badala yake tunakuwa na nia ya uungu ya Kristo. Tunakuwa tumeumbwa upya na tunakuwa na bwana mwingine katika nafasi ya yule wa zamani. Lakini kuna tofauti ya muhimu katika tabia za hawa mabwana wawili. Nia ya mwili ni bwana ambaye ni dikteta anayetawala kwa kulazimisha. Mungu kamwe hatawali kwa kulazimisha. Yeye sikuzote hutawala kwa upendo. Yeye huita, hukaribisha, hutoa; kamwe halazimishi. Kwa hiyo, tunahitaji kufanya uchaguzi binafsi na mahsusi ulio wa hakika kumtumikia Mungu kila siku. Tuko huru kuchagua kutenda dhambi wakati wowote ule. Hii ni tofauti kiasi gani na utawala wa Shetani. Mara Shetani anapokuleta chini ya uwezo wake, basi huna budi kumtumikia, uwe unapenda au la.

Wakati Yesu alipokuja katika dunia hii alisema, "Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." *Mathayo* 20:28. Hii ni kanuni kuu katika maisha ya Kristo na Mungu. Ile nia ya uungu ni mtumishi ambaye anaitumikia nia ili kuitiisha na kuitawala asili ya kibinadamu ya Mkristo, iliyoanguka, ya dhambi.

Hii haina maana kwamba Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anaweza kuitumia nia ya uungu kufanya chochote anachotaka, kwani Mungu kamwe hataweza kuitumikia dhambi. Lakini wakati tunapochagua kutii amri za Mungu za haki, basi Yeye huitumikia nia na kutupa uwezo wa kutii. Hata hivyo, Mungu hatulazimishi kumtii, wakati wote tuko huru kutomtii iwapo tutachagua kufanya hivyo.

**Katika Utendaji Halisi**

Ili kuiweka hali hii wazi zaidi tunapaswa kuufuatilia mfuatano huu wa mambo, kwanza katika suala la *Warumi* saba, na kisha *Warumi* nane. Kwa mtu wa Warumi saba linakuja jaribu la ibilisi, ambalo huvuta kwenye tamaa au udhaifu wa mwili wa kibinadamu. Katika akili yake, mtu huyu anajua kuwa hili ni kosa. Anafanya uamuzi thabiti kutofanya kosa lile na kutuma maelekezo kwenye mwili juu ya namna ya kuenenda.

Lakini katika *Warumi* saba, nia ya mwili ndiye bwana halisi. Uwezo huu ulio ndani yake hutawala tukio na kuifanya nia yake isiwe na uwezo kabisa. Matokeo yake, tamaa za mwili hazitawaliki bali hudhihirika kama dhambi ya wazi. Kwa hiyo, katika uzoefu wa *Warumi* saba nia ya mwili ndiyo kitovu cha utawala.

Katika *Warumi* nane hali ni tofauti. Majaribu yale yale huja kwenye mwili ule ule wa kibinadamu, na akili pia bado huitwa kufanya uamuzi juu ya kipi mwili utakifanya. Lakini sasa, iwapo ataamua kutokubali kushindwa na jaribu, na iwapo anayo imani kamili kuwa uweza wa Mungu ndani yake, ukiungana na uweza wa Mungu kutoka juu, utafanya uamuzi wake kutenda kazi, basi nguvu hizo kuu zitaitumikia nia kuifanya iwe na ushindi wa hakika. Mwili wa binadamu utadhibitiwa kabisa na maovu ya dhambi hayataonekana.

Ili matokeo hayo yafanikiwe, tunaweza kuona kwamba imani ndicho kitu cha muhimu kinacholeta ushindi. Kitovu cha utawala kimehamishwa kutoka katika nia ya mwili hadi kwenye nia ya mtu, lakini nia inaweza kuwa na nguvu katika juhudi yake iwapo ipo imani kwamba Bwana atafanya maamuzi yawe halisi. Kwa maneno mengine, ni lazima tutegemee uweza na nia ya Mungu kuyatimiza. Iwapo tunadhani kwamba sasa tuna nguvu za kutosha ndani yetu kuupinga uwezo wa dhambi, tutaanguka katika majaribu—hakuna kitu cha hakika zaidi ya hicho. “Mwenye haki ataishi kwa imani.” *Warumi* 1:17.

**Kuudumisha Ushindi**

Kwa hiyo kinachofuata ni kwamba tunapaswa kuudumisha uzoefu hai ambao tumeupata. Ingawa “Mwenye haki ataishi kwa imani.” *Warumi* 1:17, imani hiyo inaweza kufa na kupotezwa. Ili kuzuia hili, imani yetu inapaswa si tu kudumishwa, lakini pia lazima ikuzwe na kuimarishwa. Imani ni kitu kilicho hai na iwapo kitu hai hakiendelei kukua, basi huanza kufa.

Ili kuilea imani yetu, lazima tujilishe Neno la Mungu kila siku. Kukombolewa kutoka kwa bwana wa kale kunatajwa kama “kuzaliwa mara ya pili” katika Neno la Mungu (Tazama *Yohana* 3:3, 7; *1Petro* 1:23.) Na Petro anawaita Wakristo wapya kama “watoto wachanga waliozaliwa.” *1Petro* 2:2. Mtoto mchanga aliyezaliwa ndiyo kwanza ameanza safari ndefu ya maisha na anahitaji lishe ya kudumu ili kukua kufikia upevu kamili wa mtu mzima. Watoto wachanga waliozaliwa wanahitaji maziwa kwa ajili ya lishe yao. Hivyo baada ya kuingia katika uzoefu wa *Warumi* nane, wewe pia unapaswa kuwa, “kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.” *1Petro* 2:2.

Si tu Wakristo wachanga waliozaliwa ndio wanaohitaji kujilisha Neno la Mungu kila siku. Mkristo aliyepevuka zaidi anahitaji pia kusoma Neno kila siku ili kupata nguvu kwa siku hiyo. Bila lishe hii ya kiroho, imani zetu zitaendelea kuwa dhaifu zaidi na zaidi, mpaka tutaangushwa chini na majaribu yenye nguvu ya adui.

Kwa kawaida swali linaibuka kwamba inawezekanaje tuanguke, wakati uweza wa Mungu ni mkuu kuliko uwezo wa dhambi. Iwapo uweza huo wa uungu uko ndani yetu, basi itawezekanaje dhambi kututawala?

Mfano ufuatao unaonyesha wazi jinsi ambavyo uwepo wa uweza wa Mungu katika maisha yetu siyo uhakikisho wa moja kwa moja kwamba hatutatenda dhambi kamwe.

Jeshi lenye nguvu, kama lile lililokuwa linaongozwa na Kaisari au Aleksanda Mkuu, linakwenda kwenye mapigano. Majeshi ambayo majenerali hawa waliyaongoza yalikuwa

yenye nguvu zaidi duniani kwa muda ule, na hakuna adui aliyeweza kuyashinda. Katika jeshi kama hilo kuna sehemu mbili muhimu—jenerali wa kutoa amri na wanajeshi walio na silaha zao zote. Kwa kawaida, jenerali hana uwezo wake mwenyewe kupambana na adui mwenye uwezo mdogo zaidi anayekuja kukabiliana naye. Uwezo wa jenerali upo katika jeshi lake, na ni wakati tu lipo katika huduma yake ndipo anaweza kutarajia kusonga mbele kwa ushindi. Kwa upande wa pili, ili jeshi liweze kufanya kazi kwa ustadi na kwa manufaa, lazima liwe na ujuzi na uongozi wa jenerali. Jenerali ni nia ya jeshi na kila kitu kinategemea utendaji sahihi wa nia yake ili ushindi uwe wa hakika.

Hebu ichukuliwe kwamba jeshi lenye nguvu limesonga mbele bila kukoma na halijajua kingine ila ushindi katika njia yote. Sasa limebaki pambano moja linalopaswa kufanyika kabla ushindi wa eneo lote kupatikana. Adui mwenye jeshi dogo lisilokubali kushindwa liko chini ya vilima vidogo vidogo na makabiliano ya ana kwa ana ni ya lazima ili kupata utawala kamili wa nchi hiyo.

Lakini kwa wakati huu jenerali na wasaidizi wake wamejiamini kupita kiasi juu ya ujuzi na uwezo wao. Wanaamua kwamba kabla ya kwenda kwenye mapambano wawe na sherehe kubwa inayohusisha kula sana na kunywa usiku kucha. Hivyo jenerali na wasaidizi wake wakuu, makamanda wadogo, na maofisa, wote wanaacha jeshi kwenye kambi yake na kuyatoa masaa ya usiku kwa ajili ya sherehe yao. Matokeo bila shaka, ni kwamba kufikia asubuhi wote bado wanakabiliwa na madhara ya ulevi na kwa kweli hawajitambui.

Katika wakati huu huu, adui anachagua kufanya shambulio la ghafla dhidi ya jeshi hilo. Kwa ghafla jeshi linaamshwa na walinzi, linajikuta likiwa ana kwa ana na adui, lakini wanahitaji amri za jenerali kuyapanga majeshi yao tayari kupigana, kwani adui ni mjanja na mkali ingawa hana nguvu kama zao. Lakini kwa sababu ya hali yake ya ulevi, jenerali hawezi kufanya uamuzi na hawezi kutoa agizo hata moja kwa majeshi yanayongojea amri yake.

Ghafla jeshi linajikuta bila kamanda, bila nia, bila akili inayoongoza. Ni jeshi lenye nguvu nyingi kuliko yote duniani likikabiliana na jeshi dogo na dhaifu kuliko lenyewe, na kwa kawaida wangepata ushindi wa haraka na wa hakika. Lakini halina kiongozi, hivyo ni nani atakayepata ushindi? Bila ya shaka yoyote, adui ambaye ni mdogo na dhaifu atakuwa mshindi katika uwanja wa mapambano.

Vifanani vya kiroho vya kielelezo hiki ni kama ifuatavyo: Uwezo mkuu wa jeshi unawakilisha uweza wa Mungu katika maisha. Uweza huu ni mkubwa na hakuna chochote kinachoweza kusimama dhidi yake. Jenerali ni nia ya mtu ya kiakili na iliyoelimika katika *Warumi* nane. Adui ni mwili wa kibinadamu, usio mtakatifu na wa dhambi, ambao kupitia kwake, Shetani hufanya kazi kumwangusha na kumharibu mtu mzima.

Ingawa jeshi la kidunia linaweza kufanya kitu bila nia na maelekezo ya kamanda wake, uweza wa Mungu ndani yetu hauwezi kufanya chochote bila utendaji sahihi wa nia zetu. Kwa hiyo, wakati jaribu linapokuja na tunashindwa kufanya maamuzi sahihi na kusema "Hapana!" kwa adui, basi tutaanguka na kuwa wahanga wa Shetani kupitia mwili wetu wa kibinadamu ulioanguka.

Iwapo hatari hii haitaeleweka, tutajikuta tunaanguka chini ya uwezo wa adui, wakati ambapo maisha yetu yalipaswa kuwa wimbo wa kudumu wa ushindi dhidi ya dhambi. Kwa upande mmoja, umakini mkuu lazima utolewe kwa kazi ya nia ya mwanadamu, na kwa upande mwingine, hali ya dhambi na udanganyifu wa mwili wetu wa kibinadamu ulioanguka. Tunahitaji kuungama hali ya dhambi ya asili yetu ya kibinadamu na kutoweka tumaini lolote kwayo hata kidogo. Wakati imani yetu inapofifia, kushindwa kwetu ni kwa hakika, lakini hili si lazima litokee. Inawezekana kabisa imani yetu kudumishwa ikiwa hai, na kwa kweli ni lazima tuidumishe ikiwa hai iwapo tunataka kuishi kama Wakristo.

Wakati uhai mpya unapotolewa unakuwa mkamilifu, kama mtoto mchanga aliyezaliwa alivyo kamili. Lakini ili mtoto akue katika ukamilifu huo, ni lazima alishwe na kutunzwa. Ingawa Bwana anatoa chakula, mzazi anapaswa kumlisha mtoto chakula hicho. Mungu hamlishi mtoto moja kwa moja siku hadi siku, kwani ameikabidhi kazi hii kwa mzazi wa kibinadamu. Vivyo hivyo katika mambo ya kiroho, Mungu anatoa chakula chote cha muhimu kwenye Biblia ili kumlisha mtoto, lakini ni jukumu letu kumlisha. Mungu hatatufanyia hilo. Biblia iliyofungwa ni kama chakula kilichofungiwa kwenye stoo, ambacho hakimshibishi mtu yeyote.

**Kesha na Kuomba**

Yesu alisema, "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu." *Mathayo* 26:41.

Kuingia katika maisha ya Ukristo maana yake ni kuandikishwa katika jeshi la Bwana. Safari ya kiroho, kuanzia hapo na kuendelea, ni kusonga mbele na kupambana kila siku—siyo maburudisho. Tupo vitani, na wakati wote adui yetu yupo uwanjani akitafuta maeneo dhaifu katika tabia zetu ili aweze kutuangusha na kutuangamiza. "Mwe na kiasi na kukesha; Kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzungukazunguka, akitafuta mtu ammeze." *1Petro* 5:8.

Hakuna jeshi linaloweza kwenda vitani bila kuweka walinzi wanaokesha ili kuhakikisha kwamba adui haji dhidi yake bila kutarajia. Vivyo hivyo, kama Wakristo lazima tukeshe katika maombi kila siku. Biblia inafunua wazi mbinu zote za yule mwovu, ili kwamba tuweze kujua ni wapi na kwa jinsi gani tuweze kukesha kwa ajili yake, na kukabiliana naye kwa Neno la Mungu kabla hajafanikiwa.

**Vita ni vya Bwana**

Kanuni ya muhimu sana ambayo tunapaswa kuielewa ni kwamba jaribio lolote lisifanywe kupambana na ibilisi sisi wenyewe. Pambano kuu ni kati ya Kristo na Shetani. Iwapo tutajaribu kupigana vita vya Kristo kwa ajili yake tutashindwa. Wakati ibilisi anapotujia, lazima tumkabidhi mara moja kwa Mwokozi na kumwacha alishughulikie suala hilo. Mara tunapofanya hivi ibilisi atatukimbia, kwani anajua kwamba Kristo tayari amemshinda.

Kielelezo kingine kinaweza kusaidia kuelezea kanuni hii:

Upo katika safari katika misitu za Afrika ya kati na ni lazima upite katika eneo lenye vichaka vingi na la hatari. Wewe huijui nchi hiyo na pia wanyama wa mwitu wanaopatikana pale, lakini kiongozi mwenye uwezo na uzoefu anakupatia huduma yake. Kiongozi huyu analifahamu vizuri eneo hilo. Anaifahamu vizuri nchi hiyo na jinsi ya kushughulika na wanyama wakali. Anakuja akiwa na silaha zote zinazohitajika kwa tukio lolote.

Kadri unavyomfuata kiongozi wako, unakutana uso kwa uso na sokwe wa kutisha anayeharakisha kukushambulia mara tu anapokuona. Sasa, fikiria kwamba unaanza kupambana na mnyama huyo ukiwa mikono mitupu. Baadaye unamkumbuka kiongozi wako uliyemwajiri, na unapopigana na jitu hilo kubwa, unamwita kiongozi wako, "Haraka, nisaidie!"

Lakini ni kwa jinsi gani kiongozi huyu atakusaidia? Kwa hofu kuu atasema kwa sauti kubwa, "Rudi nyuma! Siwezi kumpiga huyo sokwe isipokuwa umeondoka njiani!" Utakuwa umeivuruga kabisa kazi ya kiongozi mzoefu na kuhakikisha kushindwa kwako isipokuwa umeondoka kando na kumruhusu kuchukua nafasi. Vivyo hivyo, lazima tumwache Kristo afanye kazi yake, na tusimzuie. Wakati adui anapokuja, tusijaribu kabisa kupigana naye, kwani "vita ni vya Bwana." *1Samweli* 17:47. "Vita si yenu, bali ni ya Mungu." *2Nyakati* 20:15.

Sisi tuko dhaifu kuliko Shetani, lakini Kristo ana nguvu zaidi. Hatuwezi kuhojiana na ibilisi. Ni Mungu pekee ndiye awezaye kufanya hivyo. Kwa hiyo, hebu wakati wote tukumbuke kumpinga ibilisi kwa uweza wa Neno wala tusijaribu kamwe kutumia nguvu zetu wenyewe. Wakati Shetani anapokujia, mwambie moja kwa moja na wazi wazi kwamba amekosea. Yule ambaye alikuwa anaitikia majaribu yale hayupo tena ndani yako. Nyakati zimebadilika na uhai mpya ndani yako haufanyi vitu hivyo tena. Mara tu ibilisi anaposikia sauti ya imani ikitangaza kweli hizi, anatoroka, na jaribu hufia mbali.

# Katika Hitimisho

Wale watakaozitumia kanuni na kuzifuata taratibu zilizoelezwa hapo juu, watakombolewa kutoka katika uwezo wa dhambi na kuwa sehemu ya mwili wa Kristo.

Mara tunapokuwa tumezaliwa mara ya pili, tunaingia katika maisha mapya. Kukamilika kwa kazi moja ni mwanzo wa kazi inayofuata. Kazi ya kuelimishwa lazima ifuate, ambayo kusudi lake ni kuiweka roho huru kutoka katika mawazo na nadharia potofu tulizojifunza katika shule ya Shetani. Mawazo na tabia potofu, ambazo tumezipata katika maisha bila kujua, kabla hatujazaliwa mara ya pili, lazima zitambuliwe na kutakaswa kutoka kwetu, moja baada ya nyingine. Badala yake, mawazo na utendaji wa haki Mungu anaotupa, sharti vikuzwe. Mara baada ya kupandikizwa mbegu njema, hiyo lazima ikue mpaka ikomae kabisa. Siku baada ya siku kutakuwepo na ukuaji thabiti iwapo muumini atajilisha Neno la Mungu lililo hai kwa maombi na kwa bidii.

Shetani atadumu kutafuta kumwondoa mtu aliyezaliwa mara ya pili kutoka kwa Kristo, na kwa huzuni, anaweza kufanikiwa nyakati fulani. Lakini hii haimaanishi kwamba ndoa yetu na Kristo imevunjika. Toba, msamaha na utakaso wa haraka vitaufanya upya ushirika wetu pamoja na Mungu; na wakati tunapojifunza mafundisho ya thamani kutoka katika makosa yetu, tutakuwa salama zaidi wakati ujao.

Kijitabu hiki siyo neno la mwisho kuhusu ukombozi kutoka katika dhambi. Kinashughulika tu na hatua ya kwanza ya kuingia katika familia ya Kristo. Maelekezo ya kwanza yamekwisha kutolewa kuhusu namna ya kudumisha uzoefu huu mpya na wa thamani wa Kikristo, lakini kazi ya matengenezo haijaelezewa kwa kina au marefu yoyote. Kitabu mwenza, *Uhuisho na Matengenezo*[*], kinashughulikia kikamilifu kipengele hiki na kinapatikana kutoka Kanisa la Kiadventista la Pumziko la Sabato[†].

Njia ya Mungu kwa kila mmoja wa watoto wake ni ushindi na amani, siyo kushindwa na mateso. Hebu kila mmoja wetu azikung'ute pingu za dhambi na kuishi kama Mungu alivyopanga tuwe. Ndipo tutafaidika na mibaraka yake mingi na kustahili kuwa vyombo ili aweze kufanya kazi kupitia kwetu kuwabariki wengine.

---

[*] *Revival and Reformation*

[†] Sabbath Rest Advent Church

Sasa au wakati mwingine ujao kila mtu hufikia hatua ambapo hutambua kwamba yeye siyo mtawala wa nafsi yake mwenyewe. Yeye ni mfungwa, amefungwa katika hali ambayo hawezi kuielezea kikamilifu.

**Kutoka Utumwa Hadi Uhuru** kinalielezea tatizo kutoka katika mtazamo wa kibiblia. Uwakilisho huu siyo maelezo marefu magumu ya kitheolojia, bali ni maelezo ya kivitendo ya somo hili. Kwanza utumwa wenyewe unaelezewa, na kisha njia kuelekea uhuru wa kweli inaonyeshwa.

Wale ambao wamepitia uzoefu wa uwezo hai wa Mungu—wanajua kwamba giza limeondolewa kutoka katika maisha yao, na siku kuu mpya imeanza. Uhuru kutoka katika dhambi umechukua nafasi ya utumwa na kukata tamaa. Muumini amekuwa sehemu ya mwili wa Kristo, na kila siku ni ushirika wenye furaha na Mkombozi mpya aliyempata. Kwa wale waliopata uzoefu wake, badiliko hili huweka alama ya hatua kubwa katika maisha. Hakuna kinachobaki vile vile tena, kwani kwa kweli mambo yote yamekuwa mapya.

Sabbath Rest Advent Church

Kutoka Utumwa Hadi Uhuru